Jumatano Agosti 16, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581404
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

SUPA JACKPOT
TZS. 1,144,172,464
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Jela** kwa kujifanya daktari na kufanya upasuaji wa ngiri maji, mgonjwa afa

UKURASA 4




KURUDIA ENZI KESI ZA UHAINI

**Ujio wa mkwamo wa demokrasia vyama vingi**

Na Ani Jozeni

TAARIFA ambazo polisi walianza kupata kigugumizi kuzithibitisha za kukamatwa na kuelekea kufunguliwa kesi ya uhaini kwa Dk.Wilibrod Slaa, mpinzani asiyehitaji utambulisho, ni doa la wazi katika mkakati wa maridhiano.

Ni kielelezo pia kuna tatizo katika mfumo wa demokrasia ya vyama vingi hapa nchini kama ilivyo kwingineko barani humu, ambako ni nadra kuona nchi inaendeshwa kidemokrasia kama inavyojulikana kwa mataifa ya Magharibi, bila bughudha.

Hapa kuna tatizo ni la kujadili, ni matukio au mfumo? Ukimwambia mkereketwa wa upinzani, au tuseme upinzani 'siasa kali' kuwa tatizo liko katika mfumo, atajitahidi kukuelewa kwa haraka na kudakia, swadakta.

Atasema shida iko katika mfumo wa katiba wakati ambapo hilo si jibu la moja kwa moja ila ni sehemu ya tatizo. Mfumo unaokwamisha siasa za vyama vingi na hata yakiwapo maridhiano ya kisiasa ni kama vile tatizo la hulka za kisiasa, halafu ukiweza utafute nini msingi wa hulka za kisiasa, kama pengine ni kwa vile ni Waafrika demokrasia siyo asili yao au ni mifumo ya kijamii.

Kutanguliza dhana ya uhaini, ambako ni hatua ya juu zaidi ya tatizo la uchochezi ambalo pia halikubaliki kisheria katika mfumo halisi wa vyama vingi ni kuchoshwa na siasa anazoendesha mtuhumiwa aliyekamatwa na polisi.

Ni kwa tayari kuhamishia mapambano kati yake na mfumo wa siasa uliopo kutoka katika majukwaa ya kisiasa kwenda mahakamani na kuwa na uhakika wa kutumia muda mrefu kwa suala hilo.

Ni kupunguza kasi ya maridhiano na kurudisha mjadala katika mfumo wa kikatiba, hivyo kukwamisha uwezekano wa maridhiano kuhusu mfumo wa katiba, kuendeleza 'mduara' wa kampeni, uchaguzi na kesi.

Kesi za uhaini zilikuwa mojawapo ya matukio makubwa ya kisiasa wakati wa awamu ya kwanza, hasa kesi za uhaini za mwaka 1971 na baadaye 1983.

Na katika matukio hayo mawili, uchovu wa kisiasa wa baadhi ya makundi ya kisiasa kwa utawala wa wakati huo ulikuwa unaonekana wazi. Baada ya Mwalimu Julius Nyerere 'kung'atuka' mwaka 1985 na maridhiano ya kuelekea mfumo wa vyama vingi kuanza, kwa kulegeza masharti ya biashara (kuagiza bidhaa nje au umiliki wa vitega uchumi, kubadilisha fedha za kigeni) na uhuru wa kujieleza kuanzisha vyombo vya habari binafsi, dhana ya uhaini ni kama ilipotea.

Katika siasa za Zanzibar suala hilo limedumu kuanzia mapinduzi yenyewe na kuanzishwa mfumo wa vyama vingi ambako kisiasa alikuwa Maalim Seif Shariff Hamada, alitolewa kuzuizini na kesi hizo kuwekwa pembeni. Ila kimsingi mahusiano yake na Serikali ya Mapinduzi hayakuondoka katika dira hiyo ya mshtakiwa wa uhaini kipindi kilichopita, au kubakia kuwa mshtakiwa mtarajiwa' wakati ambapo hapakuwa na maridhiano au serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa vile kuna maridhiano ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ( SUK) Visiwani, uchochezi kama dhana ya kisheria au itikadi ya kisiasa ya kutathmini kile wapinzani wanachokifanya umehamia Bara, sasa upinzani umepata 'mshikaki' wa kutafuna.

Hoja hii ya uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam kuanza kukwamisha maridhiano ni kielelezo kuwa sehemu isiyo ndogo ya upinzani haiwezi siasa za wastani kama zinavyotakiwa na serikali iliyoko madarakani.

Wanajua kuwa endapo watajikita katika siasa hizo itakuwa vigumu kuitingisha CCM katika hisia za watu, hivyo inatoa madai ya jumla yenye itikadi ya kilichopo hakifai, ambako kinachozungumziwa siyo sera ila uhalali wa serikali iliyoko madarakani, kwa vianzio vya kikatiba kwa jadi yao na sasa wanaelekeza nguvu kwenye mkataba wa DP World ya Dubai na Tanzania kuendesha Bandari ya Dar.

Ukiangalia mpangilio wa hoja uliopelekea kufikia kurudi katika enzi ya kesi za uhaini, unakuta kuwa hapakuwa na njia yoyote ile ambayo wakereketwa wa CHADEMA wangekwepa maandamano. Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya iliwakatalia hoja zao na wakatangaza suala la kukata rufani, na wakati mpangilio huo unaendelea, wakaeleza umuhimu wa kuanzisha maandamano yasiyoisha, na baadhi kutangaza kuiondoa serikali iliyoko madarakani kabla ya mwaka 2025.

Kwa kanuni ya kidemokrasia hilo ni lengo walilojiwekea na kwa vile mpangilio wake ni maandamano ya amani, wangeruhusiwa kuingia barabarani 'hadi kieleweke' ingekuwaje?

Fikra hiyo inaweza kutetewa na waalimu wa demokrasia ila wasidhani kuwa Afrika yote iko hivyo au itadumu hapo.

Ukilinganisha na Kenya, ni wazi kuwa siasa za Tanzania bado hazijafikia mahali ambapo tabaka tawala ambalo ni tofauti na chama tawala, ila kwa hakuna tofauti kati yao liko tayari upinzani kufanya inalotaka mradi tu hawanzi kutupa mawe. Wakianza kuruhusiwa kuandamana, mawe yakitupwa watasema watafute waliotupa mawe ila haki za walio wengi zisiguswe, yaani haki ya

Harakati za kuleta maridhiano na uhimilivu wa kisiasa zikiwakutanisha Rais Samia Suluhu Hassan na Freeman Mbowe , Mwenyekiti wa CHADEMA. **PICHA: IKULU.**

INAENDELEA UK. 14

UKURASA 11

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# 'Hatujui aliko Slaa'

• **Mdude** agoma kula, kuhojiwa mahabusu, watetezi haki za binadamu watoa angalizo... *Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**WABAINI UHUSIANO VINASABA MAUAJI YA DADA BILIONEA MSUYA**



MENEJA wa Maabara Uchunguzi wa Vinasaba vya Binadamu, Dk. Fedelis Segumba, ameieleza mahakama kuwa katika uchunguzi alioufaya alibaini kuwapo uhusiano...

## ...Samia awapa hadhari viongozi wa dini

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na maaskofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, akikata utepe kufungua rasmi jengo la kitega uchumi la kanisa hilo Safina House (picha chini), katika viwanja vya Kanisa Kuu la Roho Mtakatifu jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**




# Hoja tano za TLS kwa Rais Samia, imo Katiba mpya

UKURASA 5

**MICHEZO** YANGA HASIRA ZOTE CAF KWA ASAS J'PILI UK.24

**KATUNI** UK.6



Mkurugenzi Mtendaji Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, akizungumza na waandishi wa habari katika Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dar es Salaam jana, wakati akitoa tamko la kupinga kukamatwa watetezi wa haki za binadamu. Kulia ni Mwanasheria kutoka Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRFC), Paul Kisabo, Mwenyekiti wa JUKATA, Ananilea Nkya (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga. **PICHA: SABATO KASIKA**

# 'Hatujui aliko Dk. Slaa'

**Na Waandishi Wetu**

DICKSON Matata, wakili wa Balozi mstaafu Dk. Wilbroad Slaa, amesema hajamwona mteja wake tangu juzi alipomwacha katika Kituo cha Polisi Oysterbay, Dar es Salaam.

Amedai kuwa sasa hajui aliko mteja wake baada ya jana kumkosa katika kituo hicho cha polisi alikokuwa amewekwa mahabusu.

Dk. Slaa anadaiwa kukamatwa na Jeshi la Polisi Jumapili mchana akiwa nyumbani kwake Mbweni, Dar es Salaam kutokana na tuhuma za uhaini kwa mujibu wa Wakili Matata.

Wakili huyo alidai kuwa alipokwenda kituoni Oysterbay jana, alielezwa kuwa mteja wake amerejeshwa katika Kituo cha Mbweni lakini alipokwenda huko hakumpata.

"Hatujaonana tena na Dk. Slaa tangu nimwone mara ya mwisho juzi. Nilipofika Kituo cha Polisi Oysterbay nilitaarifiwa amerejeshwa Mbweni alikoshikiliwa kwa muda baada ya kukamatwa awali. Nilipokwenda Mbweni nako sikumkuta. Ninaendelea kufuatilia kujua aliko," alidai Wakili Matata.

Balozi Dk. Slaa anadaiwa kushikiliwa na polisi tangu Jumapili iliyopita ikiwa ni siku moja tangu kukamatwa kwa Wakili Boniface Mwabukusi na Mpaluka Nyagali, maarufu Mdude, kwa tuhuma zinazofanana - uhaini.

Wakati Wakili Matata akidai kutumwona mteja wake, Dk. Slaa, huko jijini Mbeya, inadaiwa Wakili Mwabukusi na Mdude wamegoma kula chakula tangu walipokamatwa, wakishinikiza kupelekwa mahakamani ili shauri lao lisikilizwe.

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) aliyejitambulisha kwa jina la Dk. Steven Kimondo, alidai mbele ya waandishi wa habari jijini Mbeya jana kuwa alikwenda Kituo Kikuu cha Polisi jijini kwa lengo la kuwaona Mdude na Wakili Mwabukusi na kuwasihi kusitisha mgomo huo wa kula, lakini alizuiwa kuwaona licha ya kusubiri kituoni huko kwa muda mrefu.

"Niliposikia Wakili Mwabukusi na Mdude wako Central (Kituo Kikuu cha Polisi Mbeya) nilikwenda niwaone na niwashauri wasiache kula kwa nia njema na kwa kujali afya zao. Nilifika saa sita mchana na kuondoka na saa moja jioni bila kupata bahati ya kuwaona," alidai mchungaji huyo.

Wakili wa Mwabukusi na mwanaharakati Mdude wanadaiwa kuendelea kushikiliwa katika Kituo Kikuu cha Polisi Mbeya bila kufikishwa mahakamani kutokana na sababu ambazo hazijulikani.

Wanasiasa hao wanashikiliwa kwa zaidi ya siku tatu tangu walipokamatwa mkoani Morogoro Agosti 12 usiku na kusafirishwa kwenda mkoani Mbeya kwa ajili ya kufunguliwa mashtaka ya uchochezi.

Wakili wa Mwabukusi, Philip Mwakilima, aliwaambia waandishi wa habari jana jijini Mbeya kwamba alifika katika kituo hicho cha polisi kwa lengo la kuonana na wateja wake, lakini akazuiwa. Alidai kitendo cha kuzuiwa kuwaona watuhumiwa hao ni kinyume cha sheria.

Alisema baada ya wateja wake hao kufikishwa mkoani Mbeya, Mwabukusi alichukuliwa maelezo na polisi lakini Mdude aligoma kwa masharti kuwa atatoa maelezo akipelekwa mahakamani.

Alisema kuwa mpaka kufikia jana, wateja wake walikuwa hawajapelekwa mahakamani, jambo ambalo alidai ni kinyume cha sheria na sababu za kufanya hivyo hazifahamiki.

"Sheria inaniruhusu mimi kuonana na wateja wangu nikiwa na askari anayekuwa zamu kwa wakati huo, lakini nimezuiliwa na cha kushangaza wengine wanaruhusiwa. Kinachofanyika ni kinyume kabisa cha sheria," alisema Mwakilima.

Kuhusu mwanasiasa maarufu Balozi Dk. Slaa kuunganishwa na kina Mwabukuzi, Wakili Mwakilima alidai hana taarifa rasmi, zaidi ya anazosikia kutoka kwa watu mitaani.

Baadhi ya waandishi wa habari mkoani Mbeya, wakiwamo wa Nipashe, walifika katika Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Benjamin Kuzaga kwa lengo la kujua sababu za watu hao kuendelea kushikiliwa bila kufikishwa mahakamani, wakipatiwa mrejesho kwamba kamanda alikuwa na wageni.

Wasaidizi wa Kamanda Kuzaga walidai kuwa bosi wao huyo alikuwa na mazungumzo na wageni kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.

**WATETEZI WA HAKI**

Wakati hayo yakiendelea, watetezi wa haki za binadamu nchini wamelitaka Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (DPP) kuwaachia huru bila masharti washtakiwa hao kwa kuwa hawajatenda kosa la uhaini kama inavyodaiwa.

"Kutokana na taarifa za Jeshi la Polisi pamoja na taarifa kutoka kwa mawakili wa watuhumiwa, ni dhahiri kwamba watuhumiwa walikamatwa kwa tuhuma za uchochezi, lakini tuhuma za uhaini walipewa kwenye vituo vya polisi. Sisi ni wanasheria, tunajua kesi za uhaini zina vipengele vyake," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga kwa niaba ya wenzake.

Katika mkutano na waandishi wa habari Kinondoni, Dar es Salaam jana, Dk. Anna alisema: "Hii ni kinyume na kanuni za kimataifa za upelelezi wa makosa ya jinai, unakamatwa na kosa lingine, unakwenda kupewa kule polisi una kosa lingine, hiyo inaitwa kubambikwa kesi.

"Sisi kama mashirika ya haki za binadamu tunaamini kwamba watu wanaotetea haki za binadamu wana haki ya kutoa maoni kuhusu jambo lolote katika nchi yetu ikiwamo kuhusu maboresho ya mkataba wa bandari na hawastahili kupata vitisho au kukamatwa kwa sababu ya kutumia uhuru wao uliopo kikatiba na unaolindwa na mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

"Ikumbukwe kuwa Rais alipokuwa anapokea taarifa ya tume ya kuangalia jinsi ya kuboresha taasisi ya haki jinai nchini, alisisitiza wale wanaokosoa kwa hoja, wajumuishwe kwenye tume ya mipango na siyo kuwatishia na kuwakamata."

Wakili wa THRDC, Paul Kisabo, alisema kifungu namba 39 cha Kanuni ya Adhabu kinaeleza kwamba kosa la uhaini linahusisha kitendo cha kujaribu au kumuua Rais au mtu ambaye anatangaza vita dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Watetezi hao pia walitoa rai kwa wanasiasa kuacha kutoa matamko ambayo wakati mwingine husababisha uvunjifu wa haki za binadamu.

# Samia ataka viongozi wa dini kutoyumbishwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewasihi viongozi wa dini kuendelea kuliombea taifa na kamwe wasikubali kuyumbishwa na mtu yeyote asiyelitakia mema taifa.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi wa jengo la kitega uchumi la Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Central Tanganyika, Rais Samia alisema viongozi wa dini wanapaswa kuendelea kuliombea, ili taifa lidumu katika amani, umoja na mshikamano na kamwe wasikubali kuyumbishwa.

"Niwatie ari tuendelee kuitenda kazi ya Bwana tutalipwa kwa wakati wake pamoja na kazi kubwa inayofanyika. Nihimize kazi ya kulinda maadili na kukemea maovu, muwafundishe vijana hata wakubwa wale ambao wanalitumia kanisa kufanya mambo ya ovyo naomba mkemeane.

"Tukiwatumikia watu tunamtumikia Mungu. Nitoe pongezi zangu za dhati kwa ubunifu wa jengo hili, nataka mtambue serikali itaendelea kuenzi mchango wa kanisa pamoja na kudumisha ushirikiano na taasisi zote za kidini," alisema.

Rais pia alitoa wito kwa kanisa kuwahimiza waumini kufanya kazi kwa bidii na kuchangamkia fursa mbalimbali zinazotokana na kuhamishia makao makuu Dodoma.

Kuhusu ujio wa serikali, alisema Dodoma haitajengwa kwa muda mfupi lakini jitihada za serikali zinaonekana na kuahidi mwakani atakutana na wananchi wa mkoa huo kueleza yaliyofanyika na yaliyokamilika.

Alisema jengo hilo ni hatua moja ya kujitegemea, serikali imefurahishwa kukamilika kwa mradi huo utakaochangia maendeleo ya kiuchumi. Rais Samia alisema serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na taasisi na mashirika ya kidini nchini kwa kuwa zimekuwa zikisaidia serikali kutoa huduma kwa wananchi.

Alibainisha kuwa kanisa la Anglikana tangu kuingia kwake nchini, limekuwa na mchango mkubwa kwenye sekta mbalimbali ikiwamo shule za sekondari za wasichana za Mvumi na Msalato.

Alipongeza kanisa hilo kwa kujishughulisha na shughuli za kilimo zinazounga jitihada za serikali ambazo kwasasa inatekeleza Mradi wa Jenga Kesho Iliyobora (BBT) unalenga kuwahamasisha vijana kuingia kwenye shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi.

"Serikali itaangalia namna ya kufanya kazi kwa kushirikiana na taasisi za dini ili vijana wengi waingie kwenye shughuli," alisema.

Kadhalika, alisema kanisa limekuwa likiwajali watu wenye mahitaji maalum ikiwamo watu wenye ulemavu na kwamba huo ni utumishi mwema.

Naye Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania , Dk. Maimbo Mndolwa, alisema Rais anapigwa nyundo nyingi na maneno mengi, lakini mwisho wa siku Watanzania ndio wanaopita kwenye barabara hizo na kupanda ndege na meli.

"Niwatie moyo maaskofu kazi mnayoifanya Mungu anaona msikate tamaa, pasipo na kusemwa ujue hakuna kufanya kazi, palipo na kazi yenye nguvu lazima maneno yatainuka na ushindi utainuka tutakaposimama na Mungu," alisema.

Askofu wa Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dickson Chilongani, alisema tangu amepokea uongozi kutoka serikali ya awamu ya tano Rais hajayumba wala kuteteleka.

Alisema dayosisi hiyo itatimiza miaka 91 ifikapo Novemba Mosi, mwaka huu, na ni kubwa kuliko zote duniani kwa idadi ya waumini, wachungaji na makanisa.

"Tuna wachungaji 65 wanawake na ndio dayosisi ya kwanza kuwatumia wachungaji wanawake kutoa huduma," alisema.

Kuhusu jengo la kitega uchumi la Safina, alisema limegharimu Sh. bilioni nane na litaiingizia dayosisi Sh. bilioni moja kwa mwaka.

"Kitega uchumi hiki kitasaidia kuondokana na tatizo la posho za wachungaji na sehemu ya mapato yatakayopatikana itarudi kanisani ili kuendelea kutoa huduma kwa wachungaji," alisema.

Alisema kwenye jengo hilo kuna ukumbi ambao utasaidia kukutanisha vijana wa vyuo mbalimbali na kupatiwa mada za kujadiliana za kijamii, kiuchumi, mila na desturi ili kuwa raia wema na waadilifu.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema kutokana na mkoa kupata fedha nyingi ya ujenzi wa miundombinu ya shule za sekondari, imesaidia kupokea wanafunzi mara tatu ya ilivyokuwa awali.

Alisema barabara ya mzunguko ujenzi wake umefikia asilimia 40, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato umefikia asilimia 20 na ujenzi wa Mji wa Serikali umefikia asilimia 62.5.

## HABARI KITAIFA

# Uchunguzi wabaini uhusiano vinasaba mauaji ya dada yake Bilionea Msuya

**Na Grace Gurisha**

MENEJA wa Maabara Uchunguzi wa Vinasaba vya Binadamu, Dk. Fedelis Segumba, ameieleza mahakama kuwa katika uchunguzi alioufaya alibaini kuwapo uhusiano wa vinasaba vya sampuli ya mshtakiwa Revocatus Muyela na kisu kinachodhaniwa kutumika kumchinja mdogo wa marehemu Erasto Msuya, maarufu kwa jina la Bilionea Msuya, Aneth Msuya.

Dk. Segumba alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi katika kesi ya mauaji namba 103 ya mwaka 2018. Mshtakiwa katika kesi hiyo ni aliyekuwa mke wa Bilionea Msuya aliyekuwa mfanyabiashara maarufu wa madini mkoani Arusha, Miriam Mrita.

Alidai kuwa Agosti 30, 2016 alipokea vielelezo vinne vikiambatana na barua kutoka Kamsheni ya Uchunguzi wa Kisayansi Jeshi la Polisi na alikabidhiwa na askari wa kike, lakini jina lake halikumbuki.

Shahidi huyo namba 15, akiongozwa na Wakili wa Serikali, Paul Kimweri, alivitaja vielelezo hivyo kuwa ni kisu, chupi ya rangi ya zambarau, filimbi ya chuma na sampuli ya mshtakiwa Muyela, ambavyo vilipewa alama kama kielelezo A hadi D.

Alidai kuwa maelezo ambayo yalikuwa kwenye barua ambayo iliambatana na vielelezo ilikuwa inaelekeza ni uchunguzi gani ufanywe kuhusiana na vitu

Dk. Segumba alidai kuwa barua hiyo ilitaka uchunguzi ufanyike kwa ajili ya kuonyesha uhusiano ya vinasaba ya chupi na filimbi ambayo inadaiwa ilikuwa imevuliwa kwa nguvu kutoka kwa Aneth.

Pia alidai barua hiyo ilitaka uchunguzi wa filimbi kwa sababu inadhaniwa kuwa Aneth alikuwa akiitumia na kisu kilitakiwa kufanyiwa uchunguzi kwa sababu kinadhaniwa kwamba kilimkata shingo marehemu.

Aidha, alidai kuwa sampuli hizo zilikuwa za mtuhumiwa Revocatus Muyela kutokana na maelezo ya barua kutoka kamsheni ya jeshi hilo kwamba kabla ya kufanya uchunguzi alijiridhisha kwamba sampuli hizo zilikuwa katika hali nzuri.

"Baada ya kujiridhisha kilichofuata nilianza kufanya uchunguzi kwa ajili ya mpangilio wa vinasaba na mahusiano. Nilifuata hatua zote nne na mwisho niliandika ripoti," alidai Segumba.

Shahidi huyo alidai kuwa katika uchunguzi wake alibaini kisu kilionyesha kuwepo na uhusiano wa vinasaba na kielelezo cha sampuli za mtuhumiwa Revocatus Muyela. Pia alidai kuwa chupi na sampuli za Muyela katika uchunguzi wake hakubaini kuwapo uhusiano wa sampuli ya vinasaba vya chupi.

"Baada ya kupata tafsiri ya matokeo niliyoyapata kwenye uchunguzi wangu kutokana na vielelezo nilivyopokea, niliandika ripoti yake Machi 15,2017.

"Nilipomaliza uchunguzi nilifunga vielelezo vitatu, ambapo kila kielelezo nilikifunga kwenye bahasha yake na kisha kuviweka kwenye bahasha moja, ambapo niliweka sahihi yangu na tarehe ya kumaliza uchunguzi," alidai Segumba.

Alidai kuwa vielelezo alivyofunga ni chupi, kisu na filimbi na kwamba hakufunga sampuli za Revocatus kwa sababu hakuna masalia yaliyobaki katika uchunguzi wake.

Baada ya kumaliza uchunguzi wake na kufunga vielelezo hivyo, alidai kuwa alifanya mawasiliano na kamsheni hiyo na alikwenda Sajenti John kuchukua vielelezo hivyo.

Dk. Segumba aliomba mahakama ipokee vielelezo hivyo na mahakama ilivipokea na shahidi alivifungua ili kujiridhisha kama alivyovitaja awali kuwa kisu kirefu chenye mpini mwezi, chupi ya rangi ya zambarau, filimbi ya chuma ndivyo vyenyewe.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji hayo ya wifi yake, Aneth aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada Kigamboni, Dar es Salaam, amekiri kuhusika na mauaji hayo, katika maelezo yake ya onyo.

## Watanzania kupata nafuu matibabu India

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Ndege Tanzania (ATCL), imeingia makubaliano na baadhi ya hospitali za Mumbai, India ya kutoa punguzo kwa Watanzania wanaokwenda kupata matibabu nchini humo watakaotumia usafiri wa ndege zake.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ziara yake ya India kwa ajili ya kutangaza utalii.

Alisema mtu yeyote atakayesafiri na ndege za kampuni hiyo kwenda India kwa matibabu na kuonyesha ushahidi huo kwenye hospitali hizo, atapata punguzo la gharama za matibabu atakapokuwa nchini humo.

"Tayari tuna uhusiano wa kibiashara na hospitali ya Kokilaben iliyoko Mumbai. Wasafiri wanaotumia ndege zetu hupata punguzo la gharama za matibabu wanapotibiwa katika hospitali hiyo na kuna zingine ambazo tuko kwenye hatua za mwisho za makubaliano," alisema.

Matindi alisema India ni soko jipya la utalii kwa Tanzania na ATCL inalipa umuhimu wa pekee kutokana na fursa zilizoko katika soko hilo linalokadiriwa kuwa na watu takribani bilioni 1.4.

Alisema 2019, ATCL iliongeza mtandao wake wa safari kwa kuingia kwenye soko la Mumbai na ilianza na safari moja kwa wiki kwa kutumia ndege za ATCL za abiria, sasa wana safari nne kwa wiki.

ATCL ina ndege aina ya Boeing 787- 8 Dreamliner ambazo alisema ni za kisasa, zenye utulivu angani na zenye nafasi kubwa na uwezo wa kuwafanya wasafiri wajisikie fahari na maalum na uwezo wa kampuni katika kumudu soko.



Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian linalochapishwa na kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), Wallace Mauggo (kulia), akikabidhi zawadi na barua ya pongezi kwa Mhariri Msanifu wa gazeti la Nipashe, Sanula Athanas, Dar es Salaam jana, kwa kutwaa Tuzo ya Mshindi wa Jumla wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2022. Waandishi wengine wa TGL waliotwaa tuzo mbalimbali; Shaban Njia, Rahma Suleiman, Augusta Njoji, Elizabeth Kilindi na Francis Kajubi nao walizawadiwa. Wengine ni Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (wa pili kulia) na Ofisa Utawala wa TGL, Rehema Songoro. **PICHA: JOHN BADI**

## RC ataka shule kufungwa kamera kukabili mmomonyoko wa maadili

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, ameagiza shule zote zilizopata fedha za ujenzi wa mabweni, kuanza mchakato wa kufunga kamera za CCTV ili kuimarisha ulinzi na usalama wa wanafunzi na kukabiliana na mmomonyoko wa maadili.

Mtaka alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea katika Shule ya Sekondari Yakobi wakati wa kuwapokea wanafunzi wa kidato cha tano.

Alisema kutokana na kuwapo kwa historia ya ukiukwaji wa maadili ulioripotiwa shuleni hapo, mkurugenzi wa halmashauri ya Mji wa Njombe na Wakurugenzi wa halmashauri zingine, wanapaswa kuchukua hatua za kuwatuma wataalamu wa teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA) kwa ajili ya kufunga mifumo ya kamera.

"Mabweni ya watoto yawekwe, hosteli za watoto, hatuweki kule vyumbani. Watu wa TEHAMA wanajua namna ya kuweka ili watoto wawe salama. Kamera zitafungwa hapa na ofisini kwa mkuu wa shule atakuwa anaona walimu wote na wanafunzi," alisema Mtaka.

Mtaka alisema ni lazima walimu wabebe haiba ya uzazi na ulezi maana yake atakuwa rafiki wa wanafunzi na kuwaambia yanayowasibu.

"Lakini na sisi walimu mtoto anapokuja kukushirikisha jambo libebe kwamba huyu ni mtoto wangu. Hauwezi kuwa mwalimu wa kusema ngoja nimlinde mwalimu mwenzangu kwenye jambo la ovyo ambalo unaona haliwezekani na si la kibinadamu," alisema Mtaka.

Awali, Mkuu wa Shule ya Sekondari Yakobi, Mwalimu Editha John, alisema tayari wanafunzi wa kike wa kidato cha tano wameshaanza kuripoti kati ya wanafunzi 433 waliopangiwa shuleni hapo.

Ofisa Elimu Mkoa wa Njombe, Nelasi Mulungu, alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 4.8 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni kwenye shule 12 za sekondari, hivyo kila mmoja anapaswa kuchukua hatua za kumsaidia mtoto.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Kuruthum Sadick, alisema wakati ujenzi wa mabweni ukitarajia kukamilika takribani siku tano, tayari wameandaa mazingira mengine ya kuwapokea wanafunzi.

# Jela miaka 15 kujifanya daktari, kufanya upasuaji wa ngiri maji

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masjala ya Tabora imemtia hatiani na kumhukumu kifungo cha miaka 15 Amos Mathias, maarufu Dk. Amos, kwa kosa la kumua bila kukusudia mzee wa miaka 78 aliyemfanyia upasuaji wa ngiri maji na tumbo.

Hukumu ya mahakama hiyo ilitolewa jana mbele ya Jaji Athumani Matuma baada ya mshtakiwa kukiri kosa la kuua bila kukusudia.

Amos anadaiwa kuwa katika tarehe isiyofahamika Juni 2022, maeneo ya Nhungulu, Kijiji cha Mwangoye wilayani Nzega mkoani Tabora, alimuua Lukwaja Selemani (78).

Agosti Mosi mwaka huu, alisomewa mashtaka na maelezo ya awali. Alikana kuua kwa kukusudia, lakini akakiri kuua bila kukusudia.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali, Robert Kumwembe, akisaidiana na Wakili Orester Kemilembe huku mshtakiwa akiwakilishwa na Wakili Akram Magoti.

Mshtakiwa baada ya kukiri kuua bila kukusudia, mahakama ilimtia hatiani na kabla ya kutoa adhabu, upande wa utetezi uliomba apungiziwe adhabu kwa sababu ni mkosaji wa mara ya kwanza.

Upande wa Jamhuri uliomba mshtakiwa apewe adhabu kali kwa mujibu wa sheria ili iwe fundisho kwa wengine.

Jaji Matuma alisema anatoa maelezo mafupi ya ushahidi kuhusu tukio hilo la mauaji. Alisema mshtakiwa ana umri wa miaka 35, mkazi wa Mwamala, wilayani Nzega, mkoani Tabora. Alijifanya Ofisa Tabibu.

Jaji alisema kuwa kwa kujitambulisha kuwa ni dokta, akawa anatembelea wagonjwa nyumbani na wakati mwingine wagonjwa wanakwenda nyumbani kwake kupata huduma.

"Mshtakiwa anatoa huduma za tohara, wanawake kujifungua, upasuaji wa... (alitamka neno lenye maana ya ngiri maji), kupima malaria, kuongeza maji kwa wagonjwa, kupima Virusi vya Ukimwi (VVU), kung'oa meno, kutoa ushauri wa baba na mama juu ya uzazi wa mpango na kutoa dawa kwa wagonjwa wa maradhi mbalimbali," alisema Jaji Matuma.

Alisema kuwa Juni mwaka jana, mshtakiwa alipata taarifa mzee huyo (marehemu) anaumwa ngiri maji (hernia). Alimtembelea nyumbani kwake, alimfanyia uchunguzi na kushauri familia afanyiwe upasuaji. Alimfanyia, akampa dawa za kutuliza maumivu, akaondoka.

"Baada ya kuondoka, muda mfupi alifahamishwa kwamba mgonjwa hali yake haiko vizuri, tumbo linaongezeka ukubwa, mshtakiwa alikimbia haraka. Alipofika alipendekeza afanyiwe upasuaji wa tumbo.

"Mshtakiwa alimfanyia upasuaji mgonjwa na kuondoka, oparesheni zote mbili hazikumponya zilisababisha matatizo ya afya na kufanya afya ya mzee huyo kuzorota," alisema.

Jaji Matuma alisema mshtakiwa baada ya kuona hali ya mgonjwa, alishauri ndugu wamkimbize Hospitali ya Wilaya ya Nzega. Akiwa njiani kuelekea hospitalini, alifariki dunia na mshtakiwa alikamatwa.

"Mshtakiwa alisomea uuguzi katika Chuo cha Sumve kwa miaka miwili. Alipata daraja la chini, hakuwa anaruhusiwa kufanya upasuaji.

"Nimesoma maombi kutoka kwa mawakili wa pande zote mbili. Mahakama imeyazingatia. Inampa adhabu ya kifungo cha miaka 15 jela kwa kuua bila kukusudi," alisema.

Jaji huyo alisema kila upande unayo haki ya kukata rufani ndani ya siku 60 endapo hawatoridhishwa na hukumu hiyo.

# Walalamika wanafunzi 800 kutumia vyumba vinne vya madarasa

**Na Christina Haule**, MOROGORO

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Mamboya iliyoko Kijiji na Kata ya Mamboya, Tarafa ya Magole, wilayani Kilosa mkoani Morogoro, wanakabiliwa na uhaba wa madarasa unaosababisha madarasa mawili kutumia chumba kimoja.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi kijijini huko jana, wanakijiji hao wakiwamo Chiduo Chadibwa, walisema shule hiyo ina madarasa manne ilhali ina wanafunzi 800, jambo linalosababisha wanafunzi kukaa zaidi ya 45 katika chumba kimoja kinyume cha Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014.

"Yaani wanafunzi wanakaa bila kufuata mwongozo wala sera ya elimu darasani. Darasa moja hukaa wanafunzi wa madarasa mawili. Mfano, la tatu na la nne wanaketi chumba kimoja cha darasa. Sasa hapo ni sahihi kweli na hii ndio haki elimu?" Chadibwa alihoji.

Alidai kuwa awali kulikuwa na vyumba kwa ajili ya madarasa yote, lakini ilibainika vyumba viwili vilivyokuwa vinatumika kwa ajili ya darasa la sita na saba ni vibovu, hivyo kuvunjwa. Alidai mabati yake zaidi ya 100 hayajulikani yalikopelekwa.

Ibara ya 8 ya Katiba ya Tanzania inaelekeza wananchi kushiriki shughuli za serikali yao. Katika hilo, Chadibwa alisema wanakijiji waliguswa na changamoto hiyo na kufyatua matofali zaidi ya 3,000 lakini mpaka sasa hawajapata mwongozo wowote kutoka kwa viongozi ili waanze ujenzi wa madarasa.

Mwamvita Mgulu, mkazi wa Mamboya, alisema shule hiyo pia inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa nyumba za walimu na kusababisha baadhi ya walimu kuishi vijiji vya mbali na shule na kuwapo changamoto ya ufundishaji kwa wanafunzi hasa msimu wa mvua.




Mkurugenzi Mkuu mpya wa Benki ya NCBA, Claver Serumaga, akishiriki zoezi la upandaji miti 1,000 iliyotolewa na benki hiyo, kando ya Mto Pepo katika Manispaa ya Mjini Zanzibar juzi. Benki hiyo imeahidi kutoa miti 5,000 ili kuzuia mmomonyoko wa udongo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yaadhimisha miaka 26 ikihimiza kuchangia maendeleo

**Na Maria Seme**

BENKI ya Exim Tanzania jana iliadhimisha miaka 26 ya kuwa zaidi ya benki na ikisisitiza dhamira yake ya kuendelea kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini.

Katika hafla fupi iliyofanyika Makao Makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu, alisema katika kipindi chote cha miaka 26 ya kuwapo kwa benki hiyo, imekuwa mshirika wa kutegemewa na kuchangia katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi.

"Katika kipindi cha miaka 26 iliyopita, Benki ya Exim Tanzania imebadilika na kuwa mshirika wa kutegemewa kwa wateja wetu na kutoa huduma mbalimbali zinazoendana na mahitaji yao ya kipekee," alisema.

Matundu alisema benki hiyo imekuwa ikifanya kazi kwa kuzingatia maadili, uadilifu, uaminifu na umakini, misingi ambayo imesaidia kuaminika kwa wateja wake.

"Tunatambua wajibu tulionao katika kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Tanzania na kuwawezesha watu binafsi na wafanyabiashara," alisema.

Matundu alibainisha kuwa benki hiyo imekuwa ikiwekeza katika miradi inayokuza ujasiriamali, kusaidia maendeleo endelevu na kukuza ujuzi wa masuala ya fedha.

"Tumejitolea kuinua jamii na tumefanya juhudi nyingi kuchangia maendeleo ya Tanzania kupitia programu za Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) katika sekta muhimu zikiwamo elimu na afya, na utunzaji wa mazingira.

"Kwa kufanya hivyo, siyo tu kwamba tumetimiza wajibu wetu kama benki, lakini tumekuwa mawakala wa mabadiliko chanya ndani ya jamii zetu," alisisitiza.

Alisema benki yake imeonyesha dhamira isiyoyumba katika maendeleo ya teknolojia kwa kukumbatia ubunifu wa kidijitali ili kutoa masuluhisho ya kibenki yanayofaa na salama kwa wateja wake.

Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu, Fredrick Kanga, alisema katika hafla hiyo kuwa benki hiyo iliyoanza na wafanyakazi 15 pekee katika Tawi la Samora jijini mwaka 1997, leo inaongeza idadi ya watumishi kufikia 600 nchini na zaidi ya wafanyakazi 400 katika matawi yake yaliyoko nje ya Tanzania.

"Kama benki, tunaamini kuwa mtaji wetu mkuu ni watu wetu. Tunafurahi kwamba tunaadhimisha miaka 26 ya kuwa zaidi ya benki na isingetokea bila weledi wa wafanyakazi wetu.

"Kuna benki ambazo hazijaweza kudumu kwa muda huu, lakini sisi tunaendelea kukua mwaka hadi mwaka," alitamba.

HABARI KITAIFA

# Hoja tano za TLS kwa Rais Samia

Na Romana Mallya

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kimebainisha hoja ilizowasilisha kwa Rais Samia Suluhu Hassan, zikijumuisha ushiriki wake katika mchakato wa Katiba mpya na utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai.

Juzi, Rais Samia alikutana na Rais wa TLS, Wakili Harold Sungusia, Ikulu, Chamwino jijini Dodoma. Pamoja na mambo mengine, chama hicho kiliwasilisha hoja zake kwa mkuu huyo wa nchi.

Katika mahojiano maalum na Nipashe yaliyofanyika jana kwa njia ya simu kuhusiana na kikao hicho, Wakili Sungusia, alitaja hoja nyingine ililenga suala la ushirikiano baina ya serikali na chama hicho.

**Swali: Ni hoja zipi ambazo mmeziwasilisha kwa Rais?**

**Sungusia:** Zilikuwa nyingi. Suala nzima la ushirikiano kati ya TLS na serikali, mawakili wetu wafanye biashara na sekta ya umma.

Huko nyuma serikali ni kama ilikatisha kabisa ushirikiano na mawakili binafsi. Kazi za kisheria zilifanywa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. hawakupata zile kazi za kuwakilisha mashirika ya umma.

Matokeo yake uchumi wa wakili mmoja mmoja ukayumba halafu mawakili vijana ambao wanategemea mawakili wenye uzoefu na wenyewe wanakosa mahali pa kwenda kwa sababu wazoefu hawana kipato cha kutosha.

Tunaamini ushirikiano huu wa ubia kati ya serikali na sekta binafsi usiishie kwa makandarasi au madaktari tu binafsi bali pia kuwapo na ubia na mawakili binafsi.

Hoja nyingine tuliyowasilisha kwa Rais Samia ni suala la Katiba. TLS tuna mawakili 11,600. Tunataka tushirikiane na serikali kwenye upande huo wa Katiba mpya. Tumeiomba serikali tufanye nayo kazi ya kuelimisha umma kuhusu katiba, haki za binadamu na utawala bora.


Umuhimu wetu ni mkubwa na tuna matawi 21 nchi nzima. Tunashirikiana pia na Zanzibar Law Society (ZLS) (Chama cha Wanasheria Zanzibar) nao waweze kushiriki kwa upande wa Zanzibar kwa sababu Katiba ni suala la Muungano.

Hoja nyingine ni huduma ya msaada wa kisheria ambayo hii tumezungumza kwa kirefu sana. Kuna hii programu kubwa ya msaada wa kisheria ya Mama Samia, tunaamini tukifanya kazi vizuri na serikali tunaweza kuwafikia wananchi wengi wenye uhitaji wa kupata uwakilishi wa msaada wa kisheria.

Hii ni katika kurudisha fadhila kwa jamii yetu kwa sababu tuna jukumu la kusaidia raia.

Jambo lingine tulilozungumza naye ni maboresho ya mfumo wa haki jinai. Tunajua kuna mapendekezo yametoka na TLS inaweza kutekeleza mapendekezo mengi yaliyopendekezwa na tume, lengo letu ni wananchi wapate haki.

Pia kuna zile R4 za Rais (akimaanisha falsafa ya Rais Samia (4R) ambazo anazitumia katika utawala wake zikijumuisha 'maridhiano (Reconciliation), mabadiliko (Reforms), ustahimilivu (Resilience) na kujenga upya (Rebuilding)')



Rais Samia Suluhu Hassan akimkabidhi Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Harold Sungusia, hati ya kiwanja kilichoko Arusha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za chama hicho baada ya mazungumzo yao Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma juzi. **PICHA: MICHUZI BLOG**

Hapo kwenye maridhiano na maboresho ya sheria, sera na mifumo, tunaamini tunaweza kufanya kazi kubwa sana kwenye maridhiano na hapo kwenye masuala yanayohusu maboresho ya sheria, sera na mifumo.

Na tunaziunga mkono kwa nguvu sana hizo R4 za Mheshimiwa Rais, tunaamini tutasaidia na zitatutoa.

Kuna masuala ya mfumo wa mahakama ambayo yanahitaji kuboreshwa. Tunapenda maboresho yanayotokea kule (mahakama) yaende sambamba na idadi ya mawakili.

Ofisi zetu za TLS hazina hiyo teknolojia iliyopo mahakamani. Ili iweze kuwa na tija mahakamani lazima na huku iwapo, tunahitaji maboresho hayo na huku kwetu. Tunahitaji mifumo isomane, tunahitaji pia rasilimali fedha.

**SWALI: Mnazungumziaje suala la utawala wa sheria?**

**SUNGUSIA:** Kwa kusema ukweli na bahati mbaya Watanzania wengi wanapenda kusahau mapema. Pengine ninyi waandishi wa habari mnasahau mapema. Mambo mangapi msingeweza kuyafanya katika miaka mitatu iliyopita huko nyuma.

Yapo mambo mengi usingeweza kufanya ambayo sasa hivi yanafanyika. Unataka nini tena. Hizi dosari ndogo ndogo (bila kuziainisha) ni kawaida hakuna mtu asiye na changamoto hata moja.

Tuangalie (Tundu) Lissu alikuwa anaishi wapi? Na sasa yuko wapi? Mwenyekiti wa chama hicho kikubwa kabisa cha upinzani Mheshimiwa (Freeman) Mbowe si alikuwa mahabusu? Sasa hivi yuko wapi? Si yuko uraiani?

Vyama vya siasa si vilikuwa vinafanya mikutano ya ndani? Sasa hivi si wanafanya mikutano? Vyombo vya habari si vinaongea? Ukweli ni kwamba hali imebadilika na tuna mabadiliko makubwa katika upande wa utawala bora.

Hizi dosari zilizojitokeza juzi wakati wa mkataba wa maboresho wa bandari, nchi yenye mambo mengi mazuri haiwezi kufutwa na mambo mawili au matatu yenye dosari

**Swali: Hatua gani TLS mnachukua baada ya wakili mwenzenu Boniface Mwabukusi kushikiliwa na Jeshi la Polisi?**

**Sungusia: TLS wakili yeyote awe ametu**humiwa, tuhuma hazijathibitishwa na mahakama, hatujui kama ana hatia au la au amefanya kosa vyovyote itakavyokuwa ili mradi upo kwenye kigogoro na sheria.

Sheria iliyoanzisha Tanganyika Law Society (TLS) tuliotunga si sisi na tunasema jukumu la TLS ni kuwatetea na kuwalinda mawakili ambao ni wanachama wake. Kwa hiyo sisi tuna jukumu ambalo halihitaji kupepesa macho wala kujiuliza.

Ni jukumu letu na tutalifanya kwa utaratibu wa kisheria. Atakayesema kwamba Wakili Mwabukusi kama ana hatia au hana hatia ni mahakama. Sisi kama TLS tunawajibishwa na sheria kutoa msaada kwa wakili yeyote mwanachama wetu.

Taarifa ambazo hadi jana (juzi) nilikuwa nazo kutoka kwa viongozi wetu wa Kanda ya Kusini pamoja na ofisi yetu iliyoko Mbeya, wanafuatilia kila hatua kwa hiyo sijapata taarifa za leo (jana).

Ufuatiliaji wa hili jambo unafanyika vizuri tu na viongozi wetu wa kanda pamoja na mawakili wenyewe, na yeye mwenyewe ana haki ya kuchagua mawakili wake yeye binafsi mbali na hao wa TLS inawajibika kisheria.

**Swali: Mna wito gani kwa serikali kuhusu utawala wa kisheria?**

**Sungusia:** Wito wetu ni ule ule wa kuhakikisha wanasimamia utawala wa kisheria. Utaratibu ambao upo wa kisheria usimamiwe. Sheria inasema mtuhumiwa afikishwe mahakamani basi afikishwe ili apate uwakilishi, mtuhumiwa apate haki ya kuwasiliana na ndugu zake, haki za mtuhumiwa na taratibu zote za kisheria zifuate mkondo wake.

**Swali: Je, mnaamini utawala wa kisheria umefuatwa?**

**Sungusia:** Mpaka jana kuna taratibu za kisheria zilikuwa zinaendelea, hivyo hadi sasa hatuwezi kusema umefuatwa au haujafuatwa. Tutakapoona kuna dosari tutawasiliana na mamlaka zinazohusika.

**Swali: Mnazungumziaje hati ya ardhi mliyokabidhiwa na Rais Samia?**

**Sungusia:** Tunaishukuru serikali kwa sababu lengo la chama chetu ni kujitegemea. Miradi mingi tunategemea michango ya wanachama pamoja na fedha za ufadhili.

Tunaamini kwamba kwa kuwa na eneo letu binafsi tutawekeza na kuwa na uendelevu wa huduma zetu, zikiwamo za msaada wa kisheria kwa wananchi na zinazotolewa na TLS.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
15.08.2023

TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **16.08.2023** hadi **22.08.2023** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha gari tupu wenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga** kuelekea **Bandari ya Dar Es Salaam**, gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB54202**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **23.0** |
| **Upana** | - | **Mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: **Mzenga** hadi **Bandari ya Dar Es Salaam** kupitia **Barabara ya Morogoro,** Barabara ya Mandela gari litasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217553602

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuwa na shule za bweni sawa, lakini...

**JUZI** Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alitangaza kuwapo mpango wa kuzifanya shule za kutwa za kidato cha kwanza hadi cha nne kuwa za bweni kwa nia ya kuwaepusha wanafunzi na mazingira hatarishi, vikiwamo vitendo vya ukatili.

Mpango huo wa kuwa na shule za sekondari za bweni ni mzuri ambao utawapunguzia watoto wanaoishi mbali adha ya kutembea muda mrefu hadi kufika kwenye shule zao.

Pia, utawasaidia wazazi kupunguza gharama za nauli kila siku kwa wenye watoto wanaolazimika kutumia usafiri ili kufika kwenye masomo.

Wakati akielezea nia hiyo, Mkuu wa mkoa alisema lengo lingine ni kuwaepusha wanafunzi na vitendo vya ukatili ambavyo wamekuwa wakikumbana navyo waendapo shule na wanapurudi nyumbani.

Hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti mbalimbali uliofanywa katika baadhi ya shule za bweni, vitendo vya ukatili pia vinafanyika katika shule za bweni, kama siyo kutoka kwa watu wanaowasimamia basi ni kutoka kwa wanafunzi wenzao.

Suala hili la kuwa na shule za bweni katika shule za sekondari ni zuri sana, lakini ni lazima uwekwe utaratibu wa kuwafuatilia na kuwasimamia wanafunzi hao ili wanapokuwa bweni wasikumbwe na vitendo hivyo.

Kama alivyosema mkuu huyo, nia ikiwa ni kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa bidii na kuongeza ufaulu wao.

Kwa mujibu wa Mkuu wa mkoa, tathmini ya ufaulu ya mkoa huo inaonyesha shule za kidato cha tano na sita ambazo ni za bweni zinafanya vyema kwenye matokeo ya kitaifa tofauti na shule za kidato cha nne.

Mpango huo unatokana na kuonekana shule za Dar es Salaam nyingi hazina bweni na mtaani kuwapo kwa kadhia nyingi kama foleni za barabarani na matokeo yake wanafunzi kuchelewa kufika shuleni au kurudi nyumbani baada ya masomo.

Shule za bweni zitasaidia kusimamia wanafunzi katika makuzi yao, muda wanaofika shule, walimu kuwa na muda wa kuwaongoza vyema.

Kwa mujibu wa Chalamila Mkoa wa Dar es Salaam una shule za sekondari 455 zikiwamo za serikali 182 na za watu binafsi 273.

Kati ya shule hizo kuna mfano wa shule ya wavulana ya Azania ambayo ni ya bweni, matokeo ya kitado cha sita wamepata daraja la kwanza hadi ya tatu na hakuna daraja la nne wala sifuri.

Katika mpango huo wa kuanzisha shule za bweni, gharama zitapunguzwa badala ya kuendelea kutumia umeme wa Shirika la Umeme (TANESCO), kupitia mradi wa ujenzi wa barabara za mitaa shule ziunganishiwe umeme wa nishati ya jua.

Ni kweli kuanzisha shule za bweni kuna gharama za uendeshaji ambazo lazima ziangaliwe, ikiwamo maji, umeme, chakula na mambo muhimu ya mahitaji kimsingi.

Shule za bweni zitawasaidia watoto kujifunza kujitegemea kwa kuanzisha kilimo cha bustani za mboga ambazo zitapunguza gharama kwa shule.

Pia lazima shule hizo zijifunze umuhimu wa kuhifadhi maji ili linapotokea tatizo la uhaba wa huduma hiyo wasipate tatizo la magonjwa ya kuambukiza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Jamii isizembee kuwalinda watoto

Na Queen Urio, SJMC

**LIMEKUA** jambo la kusikitisha kila mara kusikia taarifa za vifo au majeraha kwa watoto wadogo vinavyosababishwa na kukosekana kwa jitihada za kuzuia kuwa kwenye mazingira hatarishi.

Na kutokana na kukosa uangalizi mzuri kwa watoto hao, yapo matukio ambayo yamekuwa yakisikika kuwakumba kama kuzama vyooni, kwenye mashimo na madimbwi ya maji taka, kuzama mtoni au ziwani ambayo wakati mwingine husababishia vifo au majeraha ya kudumu.

Jeshi la Polisi, viongozi wa serikali za mitaa na taasisi mbalimbali wamekuwa wakifanya jitihada za kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu malezi bora na ulinzi kwa watoto pamoja na namna ya kuwasaidia wasikumbwe na mikasa ya kuhatarisha maisha yao.

Pamoja na jitihada hizo zinazofanyika kuzuia matokeo mabaya dhidi ya watoto visa hivyo bado vinaendelea kuwakumba na hata kuwaangamiza.

Kwa mfano mwaka huu pekee ni matukio mengi yameripotiwa kama, Mei 2, mtoto Slavic aliyekadiriwa kuwa na umri wa mwaka mmoja na nusu, alifariki dunia baada ya kutumbukia kisimani akiwa nyumbani kwao mtaa wa Idara ya Maji mkoani Mara wakati akicheza.

Tukio jingine lilitokea Aprili 4, mkoani Tabora, kata ya Itetemia watoto wawili wa familia moja Rashid Hamis(3) na Sada Juma 1.6 walifariki baada ya kutumbukia kwenye shimo la choo linalojengwa nyumbani kwao wakiwa wanacheza karibu nalo.

Aidha, Januari 23, Kamanda wa Jeshi la Zimamoto, Edward Lukub, alithibitisha tukio la kufariki Elina Amos (4) mkoani Geita baada ya kutumbukia kwenye kisima kirefu ambacho hakikuwa na mfuniko.

Kutokana na watoto kuendelea kukumbwa na madhila hayo, pia Umoja wa Mataifa, umekuwa ukizitaka serikali kuchukua hatua madhubuti za ulinzi wa kundi hilo na kutekeleza

**Tukio jingine lilitokea Aprili 4, mkoani Tabora, kata ya Itetemia watoto wawili wa familia moja Rashid Hamis(3) na Sada Juma 1.6 walifariki baada ya kutumbukia kwenye shimo la choo linalojengwa nyumbani kwao wakiwa wanacheza karibu nalo.**

sheria zinazohusu ulinzi wa mtoto ambazo nchi wanachama zimesaini.

Umoja wa Mataifa, umekuwa ukizitaka kuweka mikakati itakayosaidia kupunguza kama siyo kumaliza majanga yanayotokana na au kuwa katika mazingira hatarishi, uzembe ama kukosekana ulinzi wa kutosha kwa watoto hao.

Ikumbukwe kuwa sheria ya mtoto ya mwaka 2009 ni andiko linaloshughulikia masuala mengi yanayohusu haki za ulinzi wa mtoto, na inachukua mikataba na makubaliano mbalimbali ya kimataifa yanayohusu haki za mtoto.

Kwa kuzingatia jitihada hizo zinazowekwa na serikali ikiwamo Jeshi la Polisi na kama inavyoanishwa katika mikataba mbalimbali ambayo Tanzania imesaini kuhusu ulinzi wa mtoto, kuna haja ya kuzingatia na kuyatekeleza haya kwa vitendo na kwa nguvu kubwa ili kupambana na maafa kwa watoto.

Ikumbukwe kuwa kundi hili ndilo taifa la kesho, kwa maana nchi inawategemea kupata viongozi bora, wataalamu na wabobezi katika nyanja mbalimbali ikiwamo madaktari, walimu, wahandisi, waandishi wa habari weledi na nyanja zote, hivyo bila kulilinda ni kupoteza nguvu kazi.

Ni wajibu wa kila familia, mzazi, mlezi, serikali kuanzia ngazi za mitaa hadi kuu, walimu, viongozi wa dini na makundi kuungana kwa pamoja kuimarisha ulinzi kwa kundi hilo bila kujali ni wa kwako au wa mwenzio.

Kwa wale wanaozembea kwa namna moja au nyingine na kusababisha kundi hili kufikwa na madhila hayo, wasifumbiwe macho badala yake waadhibiwe ili iwe fundisho kwa wengine wanaofanya hivyo.

Vitendo hivi vya kuwaumiza watoto visichukuliwe vya kawaida, sheria zilizopo dhidi ya ulinzi wa mtoto zionekane kutekelezwa kwa vitendo na siyo kuishia vitabuni au kwenye karatasi.




Mkurugenzi wa Usimamizi wa Miliki Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Elias Mesese (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kampeni ya kudai madeni kwa wadaiwa sugu wa kodi ya nyumba za shirika. Kulia ni Meneja Habari na Uhusiano wa Shirika hilo, Muungano Saguya na Mkurugenzi wa Fedha, Adolph Kasegenya. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# NHC kuwatangaza wadaiwa sugu kwenye vyombo vya habari

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Nyumba Nchini (NHC), limeanzisha operesheni kabambe kwa ajili ya kuwanasa wapangaji wadaiwa sugu waliohama kwenda nyumba zake na deni la Sh. bilioni 18 pamoja na kuanika majina yao kwenye vyombo mbalimbali vya habari.

Pia, NHC imesema limeingia makubaliano na Kampuni ya Credit Info Bureau kwaajili ya kutangaza majina ya wadaiwa sugu ili wasiweze kupata mikopo kwenye taasisi yoyote ya fedha.

Meneja Habari na Uhusiano wa Shirika hilo, Muungano Saguya, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema wadaiwa wote wanatakiwa wawe wamelipa madeni yao ndani ya miezi mitatu na shirika limeamua kuingia mikataba na wapangaji ya kuwaruhusu kulipa madeni yao kwa awamu.

"Awali tuliwafahamisha kuwa Shirika linadai madeni yanayofikia Sh bilioni 28 na tuliwaeleza mbinu mbalimbali zinazotumika kukusanya madeni hayo ambazo zimesaidia kukusanya Sh. bilioni 5.2, lakini bado bilioni 25 na kati ya hizo, wanaodaiwa bilioni 18 ni wale waliohama kwenye nyumba zetu," alisema.

Alisema kila mpangaji anayedaiwa ahakikishe anaweka utaratibu madhubuti wa kulipa madeni yake anayodaiwa na kwa wapangaji walioopo kwenye nyumba wahakikishe wanalipa kodi na malimbikizo yao ndani ya mwezi mmoja.

"Ambaye hataweza kufanya hivyo atakuwa ameonyesha kuwa ahitaji nyumba na shirika litavunja mikataba yao ya upangaji na kuwaondoa kwenye nyumba kwa mujibu wa sheria," alisema.

"Kwa wapangaji ambao walishapewa notisi mbalimbali za kulipa kodi wanayodaiwa, utekelezaji wa notisi hizo unaendelea, kama notisi hizo zinavyoelekeza. Hivyo, shirika linawasihi watekeleze wajibu wao ili kuepuka usumbufu utakaoweza kujitokeza kwa kushindwa kutimiza wajibu huo," alisema.

Alisema kuanzia sasa mpangaji yeyote mpya hawezi kupangishwa bila kulipa amana ya pango ya miezi mitatu na kwamba hiyo itasaidia shirika kuzitumia amana hizo wanapoacha madeni na kuondoka kwenye nyumba.

Saguya alisema kwa wapangaji waliopo kwenye nyumba na ambao hawajakamilisha kulipa amana ya pango inayotakiwa wameandikiwa barua na kupewa muda mpaka Desemba 31, 2023 ili wakamilishe kulipa amana za pango vinginevyo shirika litalazimika kusitisha mikataba yao ya upangaji.

Alisema ili kuepusha madeni ya mara kwa mara, kuanzia sasa shirika halitampa mkataba mpya mpangaji ambaye atakuwa na rekodi mbaya ya kulipa kodi kwa wakati kwa kuwa kuna Watanzania wengi ambao wamekuwa wakiomba upangaji katika nyumba za shirika hilo.

Alisema wadaiwa sugu watakaokaidi maelekezo hayo ya shirika, watakuwa wameruhusu kuwatangaza katika vyombo vya habari ili mashirika na kampuni zingine zisiingie kwenye makubaliano ya kibiashara na mtu au kampuni inayodaiwa.

Alisema ili kuhakikisha kodi na malimbikizo ya madeni yanalipwa, Mkurugenzi Mkuu wa NHC ameunda Kamati ya Menejimenti ambayo itaanza kazi rasmi wiki hii ya kufuatilia madeni yote yanayodaiwa na shirika.

Alisema shirika linawashukuru wapangaji wote wanaotimiza wajibu wao wa kulipa kodi ya nyumba kwa wakati kama mikataba ya upangaji inavyoelekeza.

# TCCIA yawataka wanachama kuchangamkia fursa AfCFTA

**Na Mary Geofrey**

CHEMBA ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), imewataka wanachama wake na wafanyabiashara wote nchini kuchangamkia fursa zilizopo kwenye mkataba wa eneo huru la biashara barani Afrika (AfCFTA) kwasababu linajumuisha nchi 54.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Kaimu Rais wa Chemba hiyo, Edmund Mkwawa, alisema TCCIA imeshawajengea uwezo wanachama na wafanyabishara zaidi ya 500 na kampuni 103 kuhusu umuhimu wa kupata cheti cha uasili wa bidhaa na faida zake katika soko hilo.

"Soko hili ni fursa adhimu kwa kampuni za Afrika kufungua soko la pamoja la bidhaa na huduma. Ni fursa ya kipekee kwa wafanyabiashara wa Tanzania kulichangamkia soko hilo lenye watu zaidi ya bilioni 1.3 na kuwa mzunguko wa fedha za kimarekani trilioni 3.4," alisema Mkwawa.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi nane zilizo kwenye mpango wa majaribio wa bidhaa kupitia AfCFTA uliojulikana kama 'Guided Trade Initiative (GTI) tangu Oktoba 2022 na mpango huo unalenga kusaidia ukuaji wa minyororo ya thamani na kuratibu mazingira wezeshi ya kufanya biashara.

"TCCIA kwa kushirikiana na Sekretariati ya AfCFTA wamekuwa wakitoa mafunzo kwa wafanyabiashara wa Tanzania ili kuhakikisha wanauelewa mkataba huo pamoja na kanuni za uasili," alisema.

Alisema kampuni 105 zilizo tayari kufanya biashara kwenye soko hilo zimehifadhiwa kwenye kanzi data za chemba zikiendelea kufanyiwa ufuatiliaji wa karibu.


Kaimu Makamu Rais wa Chemba hiyo anayeshughulikia viwanda, Vicent Minja, alisema bidhaa za Tanzania zinafanya vizuri katika masoko ya kimataifa na hivyo kuwataka wafanyabishara kutosafirisha bidhaa bila cheti cha uasili kwasababu inawanyima sifa za kupata punguzo la ushuru.

Alisema soko la AfCFTA lina watu wasiopungua bilioni 1.3 linakadiriwa kuendelea kukua na kufikia Dola za Kimarekani trilioni 6.7 ifikapo mwaka 2030 na kuwahimiza wafanyabiashara kutosafirisha bidhaa nje bila cheti cha uasili.

"Tunaziomba taasisi mbalimbali za umma zikiwamo Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Wizara ya Kilimo kwa uchache wake kusaidia kufanikisha kufikia malengo," alisema Minja.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



# Mabula abainisha kukithiri migogoro ardhi kimkataba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imebaini kukithiri kwa migogoro ya ardhi ya kimkataba zaidi ya 3,000 inayochafua taswira ya wizara.

Miongoni mwa migogoro hiyo ni wa kiwanja namba 118,505 unaowahusisha Valence Matunda na Badi Nkya dhidi ya marehemu Zuberi Mwinyimvua.

Waziri Dk. Angelina Mabula, alibainisha hayo jana jijini hapa kuhusu mgogoro wa ardhi wa muda mrefu wa kimkataba dhidi ya watu hao uliopo eneo la Mbezi, mkoani Dar es Salaam.

Alisema kati ya migogoro hiyo 1,000 imeshapatiwa ufumbuzi na kamati mbalimbali zilizoteuliwa na wizara kwa ajili ya kazi hiyo katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Waziri Mabula alisema migogoro hiyo mingi inatokana na watu kuzungukana katika uuzaji viwanja, mingine inatokana na familia kuuza viwanja mara mbili na kuibuka migogoro, inayosababisha kesi mbalimbali

zinazoihusisha wizara.

"Naomba wananchi muwe makini na masuala ya kuuziana viwanja, mnapaswa kufuata taratibu za kisheria ikiwamo kuwahusisha wanasheria ili isije kuwaathiri maslahi yenu hapo baadaye," alisema Dk. Mabula.

Alifafanua kuwa kutokana na uwepo wa matatizo mbalimbali ya masuala ya kuuziana maeneo ametoa wito kwa wananchi kuwa makini katika masuala ya maeneo ya urithi kuuza bila makubaliano na kuwataka wawahusishe wanasheria ili kuepuka migogoro.

Kuhusu mgogoro wa Mbezi, Waziri Mabula alisema mgogoro baina ya wawekezaji Matunda, Nkya na mmiliki ambaye ni marehemu Zuberi Mwinyimvua, ni wa

muda mrefu toka mwaka 2007, wawekezaji hao walitakiwa kulipwa Sh. milioni 250 ili watekeleze sharti walilopangiwa na kurudisha hati ya mmiliki huyo.

Alisema cha kushangaza, Matunda ambaye ni mwekezaji aliwekewa Shilingi bilioni moja, lakini hakutekeleza agizo aliloambiwa na kwamba wizara itashirikiana na vyombo vya dola ili kuhakikisha suala hilo linafanyiwa kazi.

Kadhalika, alisema serikali imefikia hatua nzuri ya migogoro ya hifadhi dhidi ya vijiji 975 vilivyopo ndani ya eneo la hifadhi na hadi sasa wananchi wanasubiri kulipwa huku Rais akitoa ekari 2,500 ambazo wanakijiji watabakia kuishi.

Nipashe ilimtafuta Matunda kujua sababu ya kukataa kupokea fedha alizopewa ambaye alidai aliomba kulipwa Sh. bilioni 2.3 ili atekeleze sharti lao la kuwaachia kiwanja hicho.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu, akizungumza katika hafla ya maadhimisho ya miaka 26 ya benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Aomba msaada wa matibabu nchini India

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa jijini Dar es Salaam, Martha Kikwa (30), anaomba msaada wa Sh. 62,500,000 kwa ajili ya kupatiwa matibabu ya ugonjwa wa saratani ya damu nchini India.

"Ndiyo maana nimekuja kwenu ndugu zangu (Watanzania) kuomba msaada ili kuweza kushinda tatizo kubwa ambalo nimekutana nalo. Kwa kuchangia kadri utakavyoweza ili kuweza kunisaidia kupata matibabu. Na Mungu atakubariki," alisema.

Alisema amesafiri kwenda nchini humo kwa ajili ya kupata matibabu baada ya madaktari wa hospitali ya Manipap iliyopo Bangaloreoris kumfanyia uchunguzi walibaini kuwa anahitaji kupandikizwa uboho (Bone Marrow Transplant) kwa ajili ya kuponya maradhi hayo.

Martha alisema binafsi hawezi ni vigumu kupata kiasi hicho cha fedha na kwamba, imekuwa vigumu kutimiza ndoto yake ya kila siku ya kuwasaidia watu wa karibu. "… lakini kwa sasa naogopa sitakuwa na uwezo wa kufanya hivyo," alisema.

Alisema awali alipatiwa matibabu katika hospitali hiyo na kurejea nchini, baadaye alirejea tena India Aprili, mwaka huu kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi ambao ulibaini dawa alizopatiwa na madaktari baada ya kuzitumia badala ya kuponya, ugonjwa uliongezeka na kuwa saratani ya damu.



"Baada ya kurudi tena India kwa checkup (uangalizi) Aprili 2023 imeonekana dawa hazikurespond vizuri, ugonjwa uliongezeka zaidi ambao ulihitaji more expensive and aggressive treatment (gharama zaidi). Tuliweza kupata matibabu mengine chemotherapy (mionzi) kwa raundi tatu na dawa zikarespond, lakini madaktari wameshauri tiba ya kudumu ni kufanyiwa bone marrow transplant ambapo kansa hii inashambulia kiwanda cha damu," alisema.

Amewaomba watakaoguswa na tatizo hilo kutuma fedha kupitia akaunti **0152315684900** ya Benki ya **CRDB** au kwa namba **0713123392**.

# Wananchi kulipwa bilioni 5.3/- fidia ya ardhi

**Na Gideon Mwakanosya,** Songea

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 5.3 kuanza kuwalipa wananchi 900 fidia ya ardhi ya eneo la Export Processing Zone Authority (EPZA) lenye ukubwa wa zaidi ya hekari 5,000 katika Kata ya Mwengemshindo, Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Mkurugenzi wa EPZA, Charles Itembe, alisema hayo kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Kata ya Mwengemshindo uliofanyika jana kwa ajili ya uhakiki wa wananchi watakaonufaika na fidia hiyo ili waanze kulipwa.

Mkurugenzi huyo wa EPZA amewahakikishia wananchi hao kuwa madai yao yamefikia hatua ya ukamilishaji wa malipo ili wananchi waanze kulipwa na serikali ianze kuliendeleza eneo hilo baada ya wananchi wote kulipwa fidia.

Itembe alisema malipo hayo kwa mara ya kwanza yalilipwa kwa baadhi ya wananchi na awamu ya pili yatatolewa kwa wananchi ambao hawakulipwa.

Alisisitiza kuwa kabla ya kuanza kulipwa utafanyika uhakiki wa majina katika ofisi ya Kata Mwengemshindo na wanufaika watahakikiwa kwa kuleta viambatanisho vikiwamo kitambulisho, picha, pamoja na barua kutoka Serikali ya Mitaa ili malipo yalipwe kwa mtu anayestahili na yote yatalipwa kwa kupitia akaunti za benki.

Alisema, serikali baada ya kukamilisha malipo hayo na kupewa hatimiliki ya eneo hilo itaanza uwekezaji kiuchumi na kuchochea uchumi wa mji wa Songea na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla.

Naye Katibu Tawala Wilaya ya Songea, Mtela Mwampamba, aliwataka wananchi wa Kata ya Mwengemshindo kujitokeza kwenye uhakiki ili kuondoa malalamiko yanayoweza kuathiri kazi hiyo.

"EPZA wamekuja kulipa fidia ya viwanja na kila mwananchi mnufaika wa fidia hizi atalipwa kulingana na ukubwa wa eneo lake, na kila mnufaika atalipwa fidia kulingana na uthamini uliofanyika bila udanganyifu wowote," alisisitiza.

Mtathmini wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Alex Mshana, aliitaja kero kubwa ya wananchi wa Mwengemshindo kuwa ni madai ya fidia ya ardhi eneo la EPZA na sasa serikali imetoa fedha za kuwalipa.

Alisema baada ya malipo ya fidia hiyo, wananchi watatakiwa kupisha maeneo hayo ili yaendelezwe na uwekezaji wa matumizi ya umma kupitia EPZA ufanyike.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Diwani wa Kata ya Mwengemshindo, Osmund Kapinga, ameishukuru serikali kwa kutoa fedha za fidia kwa wananchi hao na kumaliza kero hiyo ya muda mrefu.



# H'shauri Simanjiro yakaa mguu sawa kumaliza kero

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, imejipanga kutatua kero na matatizo mbalimbali yaliyoko kwenye kata 18 kupitia mpango wa bango kitita.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Gracian Makota, aliyasema hayo jana kwenye kikao cha baraza la madiwani kilichofanyika katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Orkesumet.

Makota alisema kwa kutumia bango kitita wataorodhesha mawasilisho, malalamiko, kero na changamoto mbalimbali za madiwani na kuzifanyia kazi ili kuhakikisha wananchi wanapatiwa huduma za uhakika.

"Tumeandaa bango kitita ambayo italeta tija kwenye kata zetu kwa kuwa mimi na wataalamu wangu tutakaa pamoja kuhakikisha mahali penye kero na changamoto tunashughulikia," alisema Makota.

**Tumeandaa bango kitita ambayo italeta tija kwenye kata zetu kwa kuwa mimi na wataalamu wangu tutakaa pamoja kuhakikisha mahali penye kero na changamoto tunashughulikia,**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Baraka Kanunga, alimpongeza Makota kwa utekelezaji wa kasi kubwa ya maendeleo aliyoanza nayo na kuwataka madiwani wamuunge mkono.

Diwani wa Kata ya Ngorika, alitoa rai kwa viongozi wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanajipanga kuacha alama kwa jamii kwa kujenga vituo vingi vya afya wilayani humo.

Diwani wa Kata ya Mirerani, Salome Mnyawi, alisema wataalamu wa ardhi wanapaswa kupima na kuhakiki eneo walilopatiwa na Shirika la Light in Africa ili lisivamiwe na wajenge kituo cha afya.

Diwani wa Kata ya Loiborsiret, Ezekiel Lesenga, aliwataka Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA), kuweka alama za barabarani kwa kuwa hivi karibuni ng'ombe 25 waligongwa.

Naye Diwani wa Kata ya Loiborsoit, Siria Kiduya, alisema wanakabiliwa na tatizo la daraja la kuunganisha kata hiyo na Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro.

Diwani wa Kata ya Orkesumet, Sendeu Laizer, alisema mbali ya kuwa na miradi ya maendeleo kwa sasa hawana changamoto zinazowakabili.

## EWURA yaonya wananchi kuwatumia vishoka

**Na Allan Isack,** BABATI

MAMLAKA ya Uthibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetoa onyo kwa wananchi wanaowatumia vishoka kuwafungia mifumo ya umeme.

Onyo hili limetolewa na Meneja wa EWURA Kanda ya Kaskazini, Lorivii Long'idu, wakati akitoa mafunzo kwa wanafunzi wanaosoma fani ya ufundi mchundo kwa Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) juu ya umuhimu wa kuwa na leseni ili kupunguza wimbi vishoka.

Alisema kutokana na baadhi ya wananchi kuwatumia vishoka imekuwa chanzo cha kusababisha majanga ya hitilafu za umeme kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye makazi, viwanda na taasisi.

Meneja huyo alisema serikali kupitia mamlaka hiyo imeanza kutekeleza mpango unaolenga kudhibiti vishoka wanaounganisha mifumo ya umeme kwenye maeneo ya makazi na taasisi.

Alisema katika kudhibiti suala hilo wameanza kutoa mafunzo ya umuhimu wa mafundi mchundo kuwa na leseni za umeme, huku pia wakionya wananchi wanaoendelea kutumia mafundi umeme wasiokuwa na leseni zinazotolewa na EWURA.

Alisema lengo lingine la kutoa mafunzo ni kuhakikisha wanadhibiti majanga ya moto ambayo yanaweza kusababishwa na moto wa umeme kutokana na kazi zinazofanywa chini ya kiwango ambazo zilitakiwa kufanywa na wataalamu.

## Taasisi yachimba visima vya maji 74 Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

TAASISI ya Moo Maji Well Drilling Ltd imechimba visima vya maji 74 wilayani Muheza Tanga na kusambaza mabomba mitaani pamoja na kuweka matangi ya kuhifadhi maji.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Mohammed Ainahdi alisema kuwa huo ni utaratibu wa kawaida wa taasisi hiyo kusaidia jamii ili kuhakikisha kuwa wanapata maji safi na salama.

Alisema kuwa katika Wilaya ya Muheza hadi sasa wameshachimba visima 74 katika maeneo mbalimbali ya vijijini na mjini.

Mbunge wa Muheza ambaye pia ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma aliishukuru taasisi hiyo kwa kuchimba visima vya maji, kusambaza maji katika taasisi za dini, serikali na wananchi.

Hivyo, aliwataka wadau hao kuendelea na moyo huo wa kusaidia jamii hata katika maeneo mengine kwa kuwa serikali ina ushirikiano mzuri na wadau wa maendeleo.



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma (kushoto), akimjulia hali Mwenyekiti mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Muheza, Peter Jambele, aliyelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga Bombo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Ummy aagiza umakini upatikanaji dawa kituo cha afya

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amemuagiza Mganga Mkuu wa Jiji la Tanga, kuhakikisha anasimamia upatikanaji wa dawa katika Kituo cha Afya Duga.

Pia, ameutaka uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga kufanya ukarabati wa paa katika kituo hicho, ili kuepusha madhara kwa wananchi. Alitoa maagizo hayo jana alipofanya ziara ya ukaguzi wa kituo hicho na kusema suala hilo ni muhimu, hivyo wahusika wanapaswa kuhakikisha wanasimamia na kufanyia kazi.

Alisema pamoja na watumishi kufanya kazi nzuri wanapaswa kuhakikisha wanadhibiti vifo vya kinamama na watoto katika kituo hicho pamoja na upatikanaji wa dawa. Ummy ambaye pia ni Mbunge wa Tanga Mjini mbali na kufanya ziara hiyo pia alifungua shina la vijana wakereketwa wa CCM, Mtaa wa Magomeni Kirare na kutoa Shilingi milioni moja kuwaunga mkono, huku akihaidi kuwatengenezea turubai moja.

Kadhalika, alifungua ofisi ya CCM Kata ya Duga na kuahidi kuendelea kujitolea. Awali, alinunua meza tatu na viti saba kwa ajili ya ofisi hiyo, ili kuhakikisha shughuli zinafanyika kwa ufanisi na tija.

Pia, alitembelea makazi ya wazee Duga na kusema ni utamaduni aliojiwekea kila wakati kwenda eneo hilo au kutuma wasaidizi wake kuwaona wazee hao na kuwapatia misaada mbalimbali ikiwemo vyakula.



# Wakazi Kishapu wawajengea walimu nyumba za kisasa

Na Marco Maduhu, KISHAPU

WANANCHI katika Kijiji cha Muguda Kata ya Kiloleli wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, wamewajengea walimu nyumba za kisasa.

**Wamekuwa wakijengewa uwezo na Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP), jinsi ya kuibua kero ndani ya jamii na kuzitafutia ufumbuzi.**

Inaelezwa kuwa wananchi hao waliamasishwa na Kituo cha Taarifa na Maarifa (TGNP) na kuweza kuchangia fedha pamoja na vifaa vya ujenzi ili kuwasaidia walimu hao kuondokana katika mazingira magumu ya nyumba za udongo.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Lakeshi Malendeja, alieleza kuwa baada ya wananchi kuhamasishwa na kituo hicho kuchangia maendeleo kwa kujenga nyumba za walimu ili waishi katika mazingira salama, ndipo wakaguswa na jambo hilo na kuamua kuchanga fedha na kujitoa nguvu kazi na ujenzi ukaanza.

"Wananchi waliguswa na nyumba ambazo wanaishi walimu hazikuwa na uimara na haziendani na hadhi yao, baada ya kupewa elimu ndipo wakajitoa kuwajengea nyumba bora ili waishi sehemu salama na kuwapatia elimu bora watoto wao," alisema Lakeshi.

Mtendaji wa Kijiji cha Muguda, Lenard Ngalina, alisema kijiji hicho kina kaya 298, na walichanga fedha hadi Sh.milioni saba, huku Halmashauri ya Kishapu nayo iliwaunga mkono kwa kutoa Sh.milioni 26 na hatimaye kufanikisha ujenzi huo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Muguda, Simeo Kamuli, alisema shule hiyo ina walimu saba, kati yao wanne sasa hivi wanaishi kwenye nyumba bora, wamebaki walimu watatu ambao bado wanaishi katika nyumba za tope.

Alisema mwalimu kuishi katika nyumba ya tope ambayo haina ubora inamtoa katika hali ya ufundishaji mzuri wa wanafunzi, lakini kwa sasa kuishi katika nyumba nzuri ana imani ufundishaji utakuwa wa ufanisi zaidi na ufaulu kwa wanafunzi utaongezeka.

Katibu wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kata ya Kiloleli, Zacharia Pimbi, alisema wamekuwa wakijengewa uwezo na Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP), jinsi ya kuibua kero ndani ya jamii na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema baada ya kufika katika shule hiyo waliona mazingira ya nyumba ambazo wanaishi walimu siyo salama, ndipo wakazungumza na uongozi wa kijiji, kisha wakaitisha mkutano wa hadhara na kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kujenga nyumba bora za walimu.

Aidha, alisema bado ujenzi wa nyumba zingine za walimu utaendelea kupitia nguvu za wananchi kwa kushirikiana pia na serikali ili kuhakikisha walimu wote ambao wanafundisha katika shule hiyo waishi katika nyumba bora na imara.



Ujumbe wa maofisa waandamizi kutoka Wizara ya Madini, wakipatiwa maelezo ya uendeshaji wa shughuli katika kitengo cha uzalishaji kutoka kwa Kaimu Meneja wa Idara ya uzalishaji wa mgodi wa dhahabu wa Barrick Bulyanhulu, Raymond Zakayo (kulia), walipotembelea mgodini hapo, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji madini wadogo wapewa leseni

Na Shaban Njia, KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo zaidi ya 500 katika Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga wamepatiwa leseni za uchimbaji wa dhahabu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024.

Lengo ni kuondokana na adha ya kuondolewa na wachimbaji wenye mitaji mikubwa katika maeneo wanayoyaibua.

Akieleza juu ya mafanikio ya kupata leseni, mmoja ya wachimbaji waliopata leseni hizo, Maziku Wilison, alisema zimewasaidia katika kudhibiti migogoro katika machimbo.

"Tunashukuru serikali kwa hatua hii ya muhimu maana imeendelea kututambua na kutuwezesha hali ambayo inatusaidia kufanya shughuli zetu kwa uhakika, kuaminika na kukopesheka na taasisi za fedha kulinganisha na ilivyokuwa kipindi cha bila leseni," alisema

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Hamisi Katimba, alisema watahakikisha wanatengeneza mazingira rafiki ya kufanya shughuli zao hasa ya ujenzi wa vyoo na barabara ili waweze kukusanya mapato bila kuwepo kwa migogoro.

Akieleza juu ya wachimbaji waliopata leseni, Mbunge Msalala, Idd Kassimu alisema lengo ni kuhakikisha sekta ya madini inawanufaisha wachimbaji wadogo na kuondokana na adha ya kuondolewa katika maeneo wanayoyaibua wao.

Alisema wachimbaji wadogo 500 wamepatiwa leseni za uchimbaji wa madini na sasa kazi inayofanyika ni kutoa elimu kwao ikiwa ni pamoja na kuwasimamia ili wafanye shughuli za uchimbaji kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni za utunzaji wa mazingira.

Kassimu alisema hatua ya wachimbaji hao kupatiwa leseni hizo kuna punguza migogoro kati yao na wawekezaji wakubwa ambao wengi walikuwa wanayakatia leseni maeneo ya uchimbaji yanayoibuliwa na kundi hilo na kuwataka kuacha tabia ya kutorosha madini ili kuepuka kunyang'anywa leseni hizo.

Alisema serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) wanatarajia kujenga mitambo ya kuchenjua dhahabu katika mji mdogo Kata ya Segese ambapo wachimbaji wadogo wasiokuwa na mitambo watakuwa wanachenjua dhahabu zao kwa gharama nafuu, lengo likiwa ni kukusanya mapato na kudhibiti mianya ya utoroshaji.

# Daktari feki ahukumiwa kwenda jela miaka 15

Na Halima Ikunji, Tabora

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Tabora imemhukumu, Amosi Matias (35) kwenda jela miaka 15 kwa kosa la kujifanya daktari, kumfanyia upasuaji wa sehemu za siri, Lukwaja Selemani (78) mkazi wa Kijiji cha Mhungulu Mwangohe wilayani Nzega mkoani Tabora na kumsababishia umauti.

Aidha, mshitakiwa huyo anadaiwa alijifanya daktari wa binadamu kwa kufanya upasuaji wa sehemu za siri na tumbo kwa wakati mmoja na kusababisha kifo cha mgonjwa.

Akisoma hukumu hiyo jana, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Athumani Matuma alisema kuwa mshitakiwa huyo alitenda kosa hilo Juni 10, mwaka 2022 katika kijiji hicho akijifanya yeye ni daktari bila ya kuwa na cheti chochote katika kazi yake.

Jaji alieleza kuwa awali mshtakiwa huyo alikubali kutenda kosa hilo la kufanya upasuaji kwa mzee huyo sehemu mbili za mwili wake akiwa amemlaza kwenye kitanda cha udongo.

Alisema hukumu hiyo imetolewa kwa mujibu wa Sheria Kifungu cha Mauaji cha 196 na cha 197 kwa lengo la kutoa fundisho kwa yeyote mwenye kutaka kufanya kosa la namna hiyo kwa kujua ama kutokujua.

Jaji huyo alisema mgonjwa huyo baada ya kuzidiwa kutokana na upasuaji huo alianza kuvimba mwili kutokana na vifaa alivyokuwa akifanyiwa upasuaji kutokuwa salama.

Alibainisha kwamba mshitakiwa huyo pia alikuwa akitoa tiba ya kuwang'oa meno wananchi kwa gharama ya Sh. 15, 000, upasuaji Sh. 200,000.

Alisema awali mgonjwa huyo alitoa kianzio cha Sh. 150,000, lakini baada ya kufariki wanafamilia hawakuweza kumlipa fedha zilizobakia.

Vilevile ilielezwa mahakamani hapo kwamba mtuhumiwa huyo alikuwa akiwazalisha kinamama, huku akiwalaza katika chumba cha wagonjwa chenye kitanda cha udongo.

**Akisoma hukumu hiyo jana, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Athumani Matuma alisema kuwa mshitakiwa huyo alitenda kosa hilo Juni 10, mwaka 2022 katika kijiji hicho akijifanya yeye ni daktari bila ya kuwa na cheti chochote katika kazi yake.**



Ukurasa 12

**Wenye maoni tofauti chonde chonde msisahau uvumilivu wa kisiasa**



Ukurasa 13


Kinana alivyopangua mchongo wa madai ya 'kupigwa' milioni 12


# siasa

JUMATANO AGOSTI 16, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 14

**NI MKUKI KWA MOHAMED BAZOUM**
**Kutoka rais hadi mfungwa kizuizini, chakula kiduchu, tambi, wali mkavu**

KURUDIA ENZI KESI ZA UHAINI

# Ujio wa mkwamo wa demokrasia vyama vingi

**Na Ani Jozeni**

TAARIFA ambazo polisi walianza kupata kigugumizi kuzithibitisha za kukamatwa na kuelekea kufunguliwa kesi ya uhaini kwa Dk.Wilibrod Slaa, mpinzani asiyehitaji utambulisho, ni doa la wazi katika mkakati wa maridhiano.

Ni kielelezo pia kuna tatizo katika mfumo wa demokrasia ya vyama vingi hapa nchini kama ilivyo kwingineko barani humu, ambako ni nadra kuona nchi inaendeshwa kidemokrasia kama inavyojulikana kwa mataifa ya Magharibi, bila bughudha.

Hapa kuna tatizo ni la kujadili, ni matukio au mfumo? Ukimwambia mkereketwa wa upinzani, au tuseme upinzani 'siasa kali' kuwa tatizo liko katika mfumo, atajitahidi kukuelewa kwa haraka na kudakia, swadakta.

Atasema shida iko katika mfumo wa katiba wakati ambapo hilo si jibu la moja kwa moja ila ni sehemu ya tatizo. Mfumo unaokwamisha siasa za vyama vingi na hata yakiwapo maridhiano ya kisiasa ni kama vile tatizo la hulka za kisiasa, halafu ukiweza utafute nini msingi wa hulka za kisiasa, kama pengine ni kwa vile ni Waafrika demokrasia siyo asili yao au ni mifumo ya kijamii.

Kutanguliza dhana ya uhaini, ambako ni hatua ya juu zaidi ya tatizo la uchochezi ambalo pia halikubaliki kisheria katika mfumo halisi wa vyama vingi ni kuchoshwa na siasa anazoendesha mtuhumiwa aliyekamatwa na polisi.

Ni kwa tayari kuhamishia mapambano kati yake na mfumo wa siasa uliopo kutoka katika majukwaa ya kisiasa kwenda mahakamani na kuwa na uhakika wa kutumia muda mrefu kwa suala hilo.



Harakati za kuleta maridhiano na uhimilivu wa kisiasa zikiwakutanisha Rais Samia Suluhu Hassan na Freeman Mbowe , Mwenyekiti wa CHADEMA. **PICHA: IKULU.**

Ni kupunguza kasi ya maridhiano na kurudisha mjadala katika mfumo wa kikatiba, hivyo kukwamisha uwezekano wa maridhiano kuhusu mfumo wa katiba, kuendeleza 'mduara' wa kampeni, uchaguzi na kesi.

Kesi za uhaini zilikuwa mojawapo ya matukio makubwa ya kisiasa wakati wa awamu ya kwanza, hasa kesi za uhaini za mwaka 1971 na baadaye 1983.

Na katika matukio hayo mawili, uchovu wa kisiasa wa baadhi ya makundi ya kisiasa kwa utawala wa wakati huo ulikuwa unaonekana wazi. Baada ya Mwalimu Julius Nyerere 'kung'atuka' mwaka 1985 na maridhiano ya kuelekea mfumo wa vyama vingi kuanza, kwa kulegeza masharti ya biashara (kuagiza bidhaa nje au umiliki wa vitega uchumi, kubadilisha fedha za kigeni na uhuru wa kujieleza kuanzisha vyombo vya habari binafsi, dhana ya uhaini ni kama ilipotea.

Katika siasa za Zanzibar suala hilo limedumu kuanzia mapinduzi yenyewe na kuanzishwa mfumo wa vyama vingi ambako mdau muhimu wa mivutano ya kisiasa alikuwa Maalim Seif Shariff Hamada, alitolewa kuzuizini na kesi hizo kuwekwa pembeni. Ila kimsingi mahusiano yake na Serikali ya Mapinduzi hayakuondoka katika dira hiyo ya mshtakiwa wa uhaini kipindi kilichopita, au kubakia kuwa mshtakiwa mtarajiwa' wakati ambapo hapakuwa na maridhiano au serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa vile kuna maridhiano ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ( SUK) Visiwani, uchochezi kama dhana ya kisheria au itikadi ya kisiasa ya kutathmini kile wapinzani wanachokifanya umehamia Bara, sasa upinzani umepata 'mshikaki' wa kutafuna.

Hoja hii ya uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam kuanza kukwamisha maridhiano ni kielelezo kuwa sehemu isiyo ndogo ya upinzani haiwezi siasa za wastani kama zinavyotakiwa na serikali iliyoko madarakani.

Wanajua kuwa endapo watajikita katika siasa hizo itakuwa vigumu kuitingisha CCM katika hisia za watu, hivyo inatoa madai ya jumla yenye itikadi ya kilichopo hakifai, ambako kinachozungumziwa siyo sera ila uhalali wa serikali iliyoko madarakani, kwa vianzio vya kikatiba kwa jadi yao na sasa wanaelekeza nguvu kwenye mkataba wa DP World ya Dubai na Tanzania kuendesha Bandari ya Dar.

Ukiangalia mpangilio wa hoja uliopelekea kufikia kurudi katika enzi ya kesi za uhaini, unakuta kuwa hapakuwa na njia yoyote ile ambayo wakereketwa wa CHADEMA wangekwepa maandamano. Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya iliwakatalia hoja zao na wakatangaza suala la kukata rufani, na wakati mpangilio huo unaendelea, wakaeleza umuhimu wa kuanzisha maandamano yasiyoisha, na baadhi kutangaza kuiondoa serikali iliyoko madarakani kabla ya mwaka 2025.

Kwa kanuni ya kidemokrasia hilo ni lengo walilojiwekea na kwa vile mpangilio wake ni maandamano ya amani, wangeruhusiwa kuingia barabarani 'hadi kieleweke' ingekuwaje?

Fikra hiyo inaweza kutetewa na waalimu wa demokrasia ila wasidhani kuwa Afrika yote iko hivyo au itadumu hapo.

Ukilinganisha na Kenya, ni wazi kuwa siasa za Tanzania bado hazijafikia mahali ambapo tabaka tawala ambalo ni tofauti na chama tawala, ila kwa hakuna tofauti kati yao liko tayari upinzani kufanya inalotaka mradi tu hawaanzi kutupa mawe. Wakianza kuruhusiwa kuandamana, mawe yakitupwa watasema watafute waliotupa mawe ila haki za walio wengi zisiguswe, yaani haki ya

INAENDELEA UK. 14




Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea tuzo ya maridhiano kutoka kwa Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe. **PICHA: MTANDAO**

# Wenye maoni tofauti ya kisiasa chonde chonde msisahau uvumilivu wa kisiasa

**Na Mwandishi Wetu**

KUKAMATWA kwa mawakili Boniface Mwabukusi na Nyagili Mpaluka pamoja na mpinzani mkongwe Dk. Wilbroad Slaa, ni jambo linalowaelekeza Watanzania, viongozi wa kisiasa na kijamii hasa asasi za kiraia kuhubiri mambo yanayoepusha kukosekana maridhiano.

Aidha, kamata yao inayohusishwa na kupinga mkataba wa uwekezaji wa kampuni ya Dubai ya DP World kwenye Bandari ya Dar es Salaam, kuwakumbushe wanaohubiri demokrasia na uhuru wa kutoa maoni kuwa na uvumilivu wa kisiasa.

Uvumilivu wa kisiasa, ni nia ya kupanua haki za kimsingi na uhuru wa kiraia kwa watu na mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo maoni yao yanatofautiana na ya serikali au vyama vilivyoko madarakani.

Inaweza kuwa ni kanuni kuu ya demokrasia inayozingatia kuthamini haki na uhuru wa mtu binafsi, chama cha kisiasa na AZAKI kutoa maoni na kuthamini au kuleta mawazo mengine tofauti na wengine.

Kuchukua msimamo wa kuvumiliana ni mojawapo ya kazi ngumu zaidi ambayo binadamu au mwananchi hukabiliana nayo popote pale. Lakini, ni lazima ili kuishi. Inawezekana wanadamu wengi hawajazaliwa kuwa wastahimilivu, japo inabidi watu wajaribu kujifunza kuwa wastahimilivu.

Kama wawakilishi wa umma, wanasiasa na viongozi wanatarajiwa kuvumiliana na kuongoza kuwa mfano wa wanaobeba uvumilivu huo. Haina maana kuitukana au kuitishia serikali kwa kuwa popote duniani hilo halitakubalika.

Mwanasiasa anapoona amekwama hana sababu ya kuangalia mbadala ambao anaona unamletea ukurasa mwingine mgumu au utamkwamisha.

Ukweli ni kwamba kila mmoja ana wazo lake na hisia anazotaka wananchi wa kawaida na serikali na umma usikie na kutoa uzito kwa hayo yanayotoka kwenye kinywa chake, cha viongozi na wadau ambao wana tofauti za kisiasa na misimamo.

Hata hivyo, ukiwa na maoni au hisia tofauti haimaanishi kuvuka mstari au taa nyekundu na kusababisha ajali au hatari.

Wakati umefika Watanzania waonyeshe kwamba ni watu wenye ukomavu na uvumilivu wa kisiasa na kuepuka aina zote za vurugu ambazo zinaweza kuleta changamoto kwenye maridhiano ya kisiasa na kusababisha wapinzani na mawakili kufunguliwa mashtaka ya uhaini na uchochezi jambo ambalo haliwasaidii wala halijengi demokrasia ambayo wengi wanaitamani.

Halikadhalika Watanzania wakumbuke kuwa katika miezi ya hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, amezungumza vikali na kutaka kuwapo na maridhiano, amani na uelewano wakati mmoja akiungana na wapinzani wake, CHADEMA katika mkutano wa jukwaa la Siku ya Wanawake Dunia, akihimiza umoja, amani, mshikamano lakini uvumilivu na uhimilivu wa kisiasa.

> Ukweli ni kwamba kila mmoja ana wazo lake na hisia anazotaka wananchi wa kawaida na serikali na umma usikie na kutoa uzito kwa hayo yanayotoka kwenye kinywa chake, cha viongozi na wadau ambao wana tofauti za kisiasa na misimamo.

Lakini, hali ya wasiwasi inaanza tena kunakuwapo na madai ya kauli za chuki na kutishia kuiondoa serikali madarakani kabla ya 2025 yote hayo yanasababisha kuzuka kwa sintofahamu kwa upinzani ambao ulikuwa umeanza kujiimarisha kwenye majukwaa ya mikutano ya hadhara na kunadi sera zake.

Rais Samia amesisitiza juu ya masuala ya kuboresha uchaguzi, kubadilisha sheria zake na hata kuandaa katiba mpya mapema kabla ya uchaguzi wa mwaka 2025, muda wote ametoa ruksa kwa upinzani kufanya kazi vizuri na serikali yake akiwaruhusu kukosoa na kupendekeza ufumbuzi wa changamoto wanazoziona.

Tangu wakati huo, hatua yake ya kutaka kushirikiana imepunguza msuguano baina ya serikali na wapinzani tena mara kwa mara amekutana nao ili kumaliza mkwamo wa kisiasa, uliokuwa unalalamikiwa na upinzani kwa takribani miaka sita.

Suala la kuwa na siasa zenye ushindani halikwepeki lakini ni lazima kuona umuhimu wa wanasiasa wa Tanzania kuwa na uvumilivu wa kisiasa.

Demokrasia ya vyama vingi, inahitaji uvumilivu wa kisiasa. Kauli isiyo pendeza serikali lakini isiyokubalika na CCM inayotoka kwa wapinzani inaposikika kwa kigezo cha kutetea uhuru wa kujieleza na haki ya kutoa maoni ni lazima itakutana na misimamo mbalimbali. Kadhalika kwa upande wa upinzani ni vyema pia kujiepusha kuvuka mipaka au mstari mwekundu kwa pande zote kwani kutavuruga na kuleta uwezekano wa kuondoa uvumilivu na uhimilivu wa kisiasa, unaojengwa.

Ni bora kuepusha maoni ambayo yanaweza kuleta matatizo hasa hayo yanayoelezwa kutishia serikali iliyoko madarakani, ni kauli ambazo pengine duniani kote hazitakubalika.

Na siku zote wanasiasa na wadau wao wakubaliane na sharti la uvumilivu katika jamii inayofanya kazi kwa kupingana kwasababu wawili hawa hawajawahi kuwa pamoja kimitizamo, uelekeo na ufanyaji kazi, ni makundi yanayowindana kuangalia udhaifu uko wapi ili kukemea.

Kufanya uvumilivu na uhimilivu wa kisiasa ni jambo linalowezekana katika jamii ya kidemokrasia. Ni uwezo wa kujizuia usivuke mipaka lakini kukataa kuanzisha na kukuza matatizo yanayoweza kuleta uhusiano mbaya na uhasama baina ya serikali, raia na wadau wengine kutokana na matendo na kauli zinazotolewa na upande mmoja.

Tukumbuke kazi kubwa ya pande mbili hizi serikali na upinzani katika kukuza amani, itakuwa ina maana zaidi kama hakutakuwa na ghasia, kutukanana, uchochezi na kuchelewesha mipango mingine ya kuboresha katiba na kupanua demokrasia inayoandaliwa.

Matukio ya hivi majuzi ya kauli zinazochukuliwa kwa hisia kali na serikali, vyombo vya ulinzi na usalama na CCM kwa ufupi ni mfano wa mambo ambayo Watanzania hawapendi yajirudie au yaendelee.

# Kinana alivyopangua mchongo wa madai ya 'kupigwa' milioni 12

## •Ofisa maliasili ashtakiwa kwa Makamu M'kiti CCM



Makamu Mwenyekiti CCM Bara Kinana, akiwahutubia wananchi mkoani Simiyu. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa SIMIYU**

MAOFISA wa maliasili kuwapelekea viongozi fomu na kuwataka wasaini tena wakiri kuwa wamepokea Shilingi milioni 12 fedha za maendeleo ya kijiji, wakati hazijapokelewa ni baadhi ya mambo yanayomkera Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana.

Yanajiri akiwa kwenye ziara ya mikoa mitano hivi karibuni na malalamiko hayo akayapata wilaya ya Itilima mkoani Simiyu, anapotoa kipaza sauti kwa wananchi kueleza kero zao.

Baada ya ruhusa hiyo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbogo, Ntimba Mahangila, anawataja maofisa maliasili wilayani humo kuwa walimpelekea fomu na kumtaka asaini, kukiri kuwa amepokea milioni 12, fedha za maendeleo ya kijiji hicho wakati hajawahi kuziona.

Anasema fedha hizo hazijaingizwa kwenye akaunti ya kijiji jambo linalomshangaza kwa nini atakiwe kuandika barua ya kukiri kuzipokea, afanye udanganyifu?

"Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti leo hii ungekuta nimefungwa iwapo ningekubali kusaini, lakini niligoma nikasema mpaka nikahakikishe benki, iwapo fedha zimeingizwa, kufika benki kiasi nilichokikuta ni 16,000 pekee," anasema Mahangila na kuongeza:

"Fedha zilitakiwa kuingizwa kwenye akaunti tangu Aprili, lakini mpaka sasa hakuna hela nimefuatilia mara kadhaa ninapigwa chenga ...Mwenyekiti hizo hela tutazipata lini?" Anahoji.

Baada ya madai hayo Kinana anambana ofisa maliasili, kuhusu fedha hizo na kukiri kuwapo kwa suala hilo na kwamba watalishughulikia.

Makamu Mwenyekiti, anamkosoa kuwa maelezo aliyopatiwa hajaridhisha na kuhoji kwa nini wasipewe fedha hiyo wafanye shughuli za maendeleo kama walivyoahidi kuwa wanaziweka Aprili kwenye akaunti hiyo lakini mpaka sasa hazijawafikia.

"Ofisa Maliasili Wilaya anasema badala ya hela kuingia akaunti ya Kijiji zikaingia akaunti nyingine, kuna jambo, msingesema zingeishia mifukoni mwa watu," anasema Kinana.

Aidha, Kinana anampa wiki moja Ofisi ya Maliasili Wilaya ya Itilima, kurejesha milioni 12 za maendeleo ya Kijiji cha Mbogo, akiwaagiza pia Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda na Mkuu wa Wilaya ya Itilima, Faiza Salum, kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa haraka na kupewa ripoti.

Ziara hiyo aliyoianza Julai 23 imemfikisha Kondoa mkoani Dodoma, Babati Mnyara, Mara, Simiyu na Tabora akiongozana na baadhi ya wajumbe wa Halmashauri Kuu (NEC)Inalenga kufuatilia utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025, kukagua uhai wa chama na kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

**TAMBO MADIWANI**

Aidha, Kinana anawakanya wananchi kuwaomba pesa madiwani, akisema anashangazwa na madiwani kujiita waheshimiwa wakati hata mishahara hawana jambo linalowaponza huku watu wakiwafuata na kuwaomba hela.

"Madiwani wanalipwa posho, hawana mishahara lakini nao eti wanajiita waheshimiwa, kwa sababu ya hiyo, mtu ana shida binafsi anakwenda kwa diwani ampe pesa, anauguliwa diwani agharamie matibabu, ana safari zake binafsi amlipie, akisema hana inakuwa nongwa unatishiwa tutakukata 2025," anasema Kinana.

Kadhalika, anasema wabunge wa nchini hii ndiyo wanaolipwa mshahara mdogo kuliko wengine wote wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iwe Congo, Kenya, Uganda, Rwanda na Sudan Kusini ukiangalia mishahara ya wenzao iko juu kuliko ya Tanzania.

"Tukisema tuwaongezee mtasikia kelele zake. Wabunge wakirudi jimboni kila mtu hodi anataka apewe hela, wakati mwingine mtu anafunga safari nauli hana mbunge ndiye ampe, akisema hana, inakuwa nongwa anaambiwa tutakutana 2025, Si sawa hata kidogo," anaonya.

**ACHENI KUJIPITISHA**

Anasema baadhi ya wanachama wameanza kujipitisha kutaka uongozi wakati waliopo hawajamaliza muda, akitaka waache.

Anawataka washirikiane katika shughuli za maendeleo badala ya kuanza kusaka uongozi mapema wasubiri muda ukifika.

Anasema kama wabunge na madiwani wanafanya kazi vizuri hakuna sababu ya kubadilishwa jambo la msingi ni wananchi kuwapima kutokana na maendeleo wanayowafanyia.

"Kero ya mtu anapitapita kutaka ubunge aliyepo hajamaliza muda wake sio jambo jema waachwe wamalize chama kitatangaza utaratibu kwani nini mbunge ashindwe kufanya kazi kisa mmeanza kampeni mapema ..." anaonya.

> "Madiwani wanalipwa posho, hawana mishahara lakini nao eti wanajiita waheshimiwa, kwa sababu ya hiyo, mtu ana shida binafsi anakwenda kwa diwani ampe pesa, anauguliwa diwani agharamie matibabu,

Anasema wananchi hao ndio wanaowapigia kura, hivyo ni muhimu wakapewa kipaumbele katika kutatua kero zao kama ilani inavyowaelekeza.

**ANGALIZO WAPINZANI**

Kinana anawashauri na kuwakumbusha wapinzani kuheshimu maridhiano ya kisiasa yaliyotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akionya matusi, kejeli na dharau dhidi kiongozi wa nchi zinapaswa kuepukwa ili kutoa fursa ya kuendeleza maridhiano na kuijenga Tanzania kwa pamoja.

"Niwasihi hatukatai mtoe hoja, mseme yale mnayotaka lakini kwa uungwana, zungumzeni kwa busara, jengeni hoja," anasema Kinana.

Kusema Rais ana akili za matope au ameuza bandari, wewe sema mkataba huu haujakaa vizuri, utaeleweka, toa hoja kwa nini hauko vizuri, upande wa pili watasema umekaa vizuri, lakini ukisema mkataba huu hata kichaa hawezi kuubali, maana nyingine unatuambia sisi sote ni vichaa."

"Rais mstaafu Benjamini Mkapa kasemwa, Jakaya Kikwete kasemwa na John Magufuli kasemwa. Sasa niwasihi Watanzania kudumisha umoja na mshikamano, kupokea kwa mikono miwili, utaratibu huu wa maridhiano ambao Rais ameuridhia kwa kupenda kuweka amani na umoja kwenye nchi yetu."

Anawataka baadhi ya wanasiasa wasifikiri kwa kutukana, kukejeli, kudharau ndiko kutafanya hoja zao zikubalike kwa haraka bali zitatupiliwa mbali.

**HAKUNA KUYUMBA**

Kiongozi huyo amewataka wana CCM wasikubali kuyumbishwa na maneno ya wapinzani badala yake wajikite kwenye malengo yao, na kwamba chama hicho kinalenga kuendelea kushika dola, hivyo wanajukumu kuhakikisha ilani natekelezwa kikamilifu.

"Nataka nizungumze jambo moja, ni kweli wenzetu ajenda zao ni za msimu, sisi ahadi zetu ni za kudumu, tuna mkataba na wananchi kupitia ilani, tukiteteraka na kutoka kwenye malengo tutapotea, jeshini vita ina kanuni 10, ya kwanza ukitaka kushinda inasema chagua lengo na ulishikilie usitoke nje ya malengo yako," anasema Kinana.

"Tembeeni kifua mbele, muiseme serikali yenu vizuri, chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, amefanya mengi mazuri, tunapomtaja taja Rais tunampa sifa ambazo anastaili yapo mengi kimaendeleo kila kata, wilaya na mkoa."

Aidha, Kinana anasema Rais Samia ametengeneza utaratibu mzuri wa makusanyo ya ndani na mwaka huu yamevunja rekodi tangue Uhuru, haijawahi kutokea.

Anasema makusanyo hayo yamefikiwa kwa sababu ya mpango mzuri, bila kashikashi, kutishana, kuwekana ndani na watu wamekubali kulipa kodi na ada mbali mbali.

"Sio hivyo tu Rais amepata misaada mingi kutoka nje, ameaminika, kutokana na kauli na vitendo vyake na namna anavyoendesha serikali," anasema Kinana.

### NI MKUKI KWA MOHAMED BAZOUM

# Kutoka rais hadi mfungwa kizuizini, chakula kiduchu, tambi, wali mkavu

• Watetezi wake wakwama sasa kushtakiwa kwa uhaini

**Na Gaudensia Mngumi**

KUNA usemi kuwa mkuki kwa nguruwe mtamu lakini ukipigwa kwa mwanadamu mchungu, ndicho kinachoendelea kwa kiongozi wa Niger Mohamed Bazoum,

akichaguliwa kwenye uchaguzi mkuu wa 2021, 'alichomwa mkuki' ikimaanisha kuwa alipinduliwa na kugeuzwa kuwa mfungwa wa kisiasa aliyewekwa kizuizini nyumbani kwake.

Ni katika taarifa ya video, mjeshi aliyetambulika kama Kanali-Meja Amadou Abdramane na wanajeshi kadhaa wanajitangazia uongozi:

"Tumeamua kukomesha utawala mnaoujua." Kisa? Anataja kuzorota kwa hali ya usalama nchini na kushamiri umaskini, uchumi kudorora, kuongeza vikundi vya uuaji na jamii hiyo kuzidi kuwa taabani licha ya kunuka utajiri."

Viongozi wa kijeshi waliionyakua madaraka nchini Niger katika mapinduzi hayo yasiyokuwa ya kumwaga damu, wanatangaza rasmi kumshtaki Mohamed Bazoum, wakati wowote kuanzia sasa.

Kiongozi huyo ambaye yuko kizuizini atafunguliwa mashtaka ya uhaini mkubwa kutokana na mawasiliano yake na wakuu wa nchi za kigeni na mashirika ya kimataifa, kuipinga hatua ya kupinduliwa akiomba msaada arudishwe ikulu.

Msemaji wa serikali Kanali Amadou Abdramane, anasema katika taarifa yake inayosomwa kwenye televisheni ya taifa jioni ya Jumapili kwamba "mamlaka ya kijeshi imekusanya ushahidi unaohitajika kumfungulia mashtaka rais aliyeondolewa madarakani...kwa uhaini mkubwa na kudhoofisha usalama wa ndani na nje wa Niger."

Abdramane pia anasema kulikuwa na kampeni ya upotoshaji dhidi ya serikali kujaribu "kufuta suluhisho lolote lililojadiliwa kuhusiana na mgogoro ili kuhalalisha uingiliaji wa kijeshi



wa ECOWAS.

Mmoja wa viongozi wa kimataifa anaozungumza nao Bazoum ni Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony J. Blinken, wakijadili masuala kadhaa na kiongozi huyo, akiomba kuungwa mkono na Marekani ili kurejesha Niger kwenye utawala wa kidemokrasia unaofuata katiba.

Marekani pia ikasisitiza kuwa usalama Rais Bazoum na familia yake ndilo jambo la muhimu zaidi.

Mnamo Julai 26, 2023 mapinduzi ya kijeshi yalitokea Niger baada ya walinzi wa rais kumkamata Bazoum, na kamanda mkuu wa kikosi cha walinzi wa rais huyo, Abdourahamane Tchiani, kujitangaza kuwa kiongozi wa mapinduzi na mkuu mpya wa kijeshi na nchi pia.

Viongozi hao wa mapinduzi baada ya kumpindua Bazoum na kuivunja serikali iliyochaguliwa aliyokuwa anaiongoza kuanzia 2021, hatua yao inalaaniwa na mataifa yenye nguvu duniani na nchi jirani ya Afrika Magharibi ECOWAS, ambazo zimeanzisha kikosi cha kijeshi ambacho kinaweza kuingilia kati kumrejesha Bazoum nadarakani.

Hatari ni kubwa si kwamba ni hatima ya Niger iliyo mzalishaji mkuu wa uraniam na mshirika wa Magharibi katika vita dhidi ya waasi na magaidi lakini ushawishi wa mataifa hasimu ya kimataifa yenye maslahi ya kimkakati katika Ukanda wa Sahel.

Mataifa yaliyo kwenye ukanda wa Sahel ni pamoja na Burkina Faso, Cameroon, Chad, Gambia, Guinea, Mauritania, Mali, Niger, Nigeria na Senegal.

Umoja wa Afrika (AU), wa Ulaya (EU), Marekani na Umoja wa Mataifa (UN) wote wanaeelza wasiwasi wao kuhusu hali ambayo Bazoum inahifadhiwa.

**LAZIMA KUJIUZULU**

Chama cha siasa cha Bazoum kimesema familia yake haina maji ya bomba, chakula safi wala madaktari na Bazoum anaiambia shirika la haki za binadamu la Human Rights Watch kwamba mwanawe anahitaji kuonana na daktari kwa sababu ya ugonjwa wa moyo.

Ripoti za vyombo vya habari zinaeleza kwamba familia hiyo imedaiwa kunyimwa chakula na maji ya kutosha.

Binti wa Bazoum, Zazia Bazoum analiambia gazeti la The Guardian kwamba jamaa zake wanakabiliwa na upungufu wa chakula na wanaishi kwa kula wali usio na mboga na tambi.

"Umeme umekatwa wakati chakula kilijaa kwenye friji na kikiendelea kuoza baada ya zaidi ya wiki mbili. Wafungwa wote watatu wamepungua uzito, huku kaka yao akipungua kilo 10," anasema Zazia.

"Unaelewa kuwa huwezi kula wali na tambi pekee siku zote, mchana na usiku," Zazia Bazoum analiambia gazeti la The Guardian. "Kwa hivyo kwa afya zao, ni hatari. Hawana hata maji safi ya kunywa na gesi kwenye jiko lao itamalizika hivi karibuni pia." Anaongeza.

Anaamini viongozi wa mapinduzi wananuia kumlazimisha baba yake kutia saini barua ya kujiuzulu. "Haya ni mateso," anasema Zazia.

**MAMBO YALIVYOMGEUKA**

Kabla ya kutangaza kumshtaki kundi la wanazuoni wa Kiislamu wa Nigeria waliokutana na kiongozi wa mapinduzi ya Niger walisema jenerali huyo amekubali kufanya mazungumzo ya moja kwa moja na kutatua mzozo kati ya viongozi wa Afrika Magharibi.

Sheikh Abdullahi Bala Lau, ambaye aliongoza ujumbe wa Nigeria, alitoa tangazo hilo siku moja baada ya kundi lake kufanya mazungumzo na Jenerali Abdourahamane Tchiani jijini Niamey.

**MITANDAO**

# UJIO WA MKWAMO WA DEMOKRASIA VYAMA VINGI

**INATOKA UK. 11**

kuandamana bila kuomba kibali polisi.

Na bila kuwapo hatari ya kuzuiwa kwa wanaharakati au viongozi wa chama husika pale watakapoitisha maandamano.

Tatizo la wanaharakati nchini ni kuwa wanakazania kuona tatizo katika mfumo wa katiba, kwa sababu wataalamu wa elimu ya siasa waliowahi kusikika ni wale ambao kimsingi ni wanasheria, ambao miaka ya karibuni wamekuwa hasa ni watetezi wa haki za binadamu.

Wanajua kunukuu vifungu kandamizi kwa mfano kufunguliwa kesi siyo ya uchochezi kama ambavyo ingedhaniwa ya uhaini. Ni kusema kulikuwa na mipango halisi kutaka kupindua serikali na siyo kutaka mabadiliko uchaguzi mkuu ujao kama baadhi yao walivyodiriki kusema, wasijue wanatoa nafasi kwa wanaohofu maridhiano 'kuchomeka' kesi.

Haitakuwa rahisi kujadili mwelekeo wa fikra ya harakati kwani fikra hii si ya Tanzania peke yake bali Afrika nzima, kuwa kinachotakiwa ni demokrasi ya vyama vingi na zaidi ya hapo ni kuandaa mkutano wa katiba kuainisha kila kipengele kinachohitaji kuondolewa, au kuandika mpya kama walivyojaribu wakati wa awamu ya nne.

Unaweza kusema kuwa ni 'kuiga tembo kunya' kwani nchi kadhaa zinafanya hivyo na sisi tunaweza pia. Wasichotaka kuangalia ni tofauti za mfumo wa jamii na hasa umiliki wa nyanja za uchumi, kuwa kwa wenzetu kuna tabaka tawala la kibiashara ambao wakipata madaraka ya kisiasa ni jambo jema kwa ndilo kundi linaloumga mkono mgombea fulani.

Ila maslahi ya tabaka hilo, kwa vile ni mapana na takriban njia zote muhimu za uchumi ziko mikononi mwao, haijalishi ni kikundi gani cha wanasiasa kiko madarakani, kwani mfumo wenyewe wa mali binafsi na mwendelezo wa sera hiyo hayatakuwa mashakani.

Tanzania tabaka tawala siyo linalofanya biashara ila lililohodhi mamlaka ya kiuchumi ya mashirika takriban 400 ya umma ambako ni machache yenye hisa zake zimewekwa katika soko la mitaji.

Hili ni tabaka linalotegemea serikali kwa asilimia 100 kwa maslahi yake na wanachelea upinzani uchukue madaraka ufagie zaidi ya watu 5,000 katika mashirika hayo na maeneo mengine serikalini, ambao wana jamaa zao na washirika wengine.

Kwa maana hiyo upinzani hapa nchini unatwanga maji kwenye kinu kutaka kuwe na demokrasia pana lakini hata siku moja hawajawahi kutaka ubinafsishaji.

Kwa lugha nyingine hawakati mabadiliko ya kina ya uchumi ila wanatamani mabadiliko ya kisiasa 'kuketi mezani kula' au kuwaondoa 'wanaokula' sasa.

Ndiyo hapo wanajitolea kwa udi na uvumba 'kufa' na huo mkataba kwani endapo hawatatumia mwanya huo wa mashaka kuhusu serikali nafasi hiyo hairudi tena.





# Vijana watakiwa kutojihusisha na mambo ya ovyo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, amewataka vijana kutokubali kutumika kwa kujiingiza katika mambo yasiyo na tija.

Badala yake wametakiwa wajishughulishe katika shughuli za kiuchumi za uzalishaji mali kama kilimo ili kuinua vipato vyao. Alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na vijana wa Mkoa wa Singida kwenye maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani.

Alisema serikali imeanzisha mradi wa BBT unaolenga kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo kwa kuwapatia mafunzo maeneo ya mashamba, hivyo ni wakati sasa kwa vijana kuchangamkia fursa hiyo.

Dk. Mganga alisema mambo ya kushinda kwenye mitandao ya kijamii na kuilaumu serikali kwamba haiwapi fursa wanapoteza muda wa kufanya mambo ya msingi ya maendeleo.

"Kuna fikra potofu imejengeka kwamba kilimo ni kazi inayofanywa na watu ambao hawajasoma na maskini hayo mambo siyo ya kweli kwani hata watumishi nao wanalima na wakifanikiwa katika kilimo watu wanabaki kusema ni mafisadi kumbe kilimo ndio kimewainua," alisema.

Dk. Mganga alisema serikali imeendelea kuleta miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Singida ambapo ilipokea Sh.bilioni 26.6 kwa ajili ya sekta ya elimu na afya na vijana wenye ujuzi kama ujenzi, upasuaji, ufundi chuma na mama lishe walipata ajira kupitia miradi hiyo.

Aliongeza kuwa serikali imetoa mikopo kwa vikundi vya vijana isiyo na riba kupitia mapato ya ndani ambapo vikundi 51 vya vijana walipatiwa Sh.milioni 274.2 na kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana zilitolewa Sh.milioni 118.6 kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

"Mkoa wa Singida unazo fursa nyingi za kiuchumi ambazo tukizitumia tunaweza kujikwamua kiuchumi fursa hizo ni kama ufugaji kuku wa asili ambapo soko kubwa lipo mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na ndani ya Singida," alisema.

Naye Ofisa Vijana Mkoa wa Singida, Frederick Ndahani, alisema katika kongamano hilo la vijana wamefundishwa fursa wanazoweza kuzichangamkia ili kujikwamua kiuchumi.

Ndahani alisema vijana wa Mkoa wa Singida wataendelea kufanya kazi kwa bidii na kulinda amani na umoja na kwamba hawatakuwa tayari kutumika na wanasiasa kuvuruga amani ya nchi. Alisema: "Sisi kama vijana wa Mkoa wa Singida tunaiahidi serikali tutaendelea kulinda amani na umoja katika nchi yetu hatupo tayari kutumika na vyama mbalimbali vya siasa na wanaharakati wanaotaka kuvuruga amani kwa maslahi yao binafsi."

# Wadau washauri Afrika iwekeze zaidi kwenye utafiti mbegu asili

**Na Mwandishi Wetu**

NCHI za Afrika zimeshauriwa kuwekeza katika utafiti wa mbegu asili kwa kuwa zina lishe bora, uhakika wa chakula na usalama kwa afya ya mtumiaji.

Ushauri huo umetolewa na wadau wa mbegu asili kutoka nchi 25 za Bara la Afrika, Marekani na Ulaya waliokutana jijini Dar es Salaam kwa siku tatu kujadili hatma ya mbegu asili katika nchi zao na dunia kwa ujumla.

Akizungumza katika mkutano huo, Paul Chilewa kutoka Mwamvuli wa Asasi za Kuendeleza Kilimo Hai Tanzania (TOAM), alisema mkutano huo ambao umehusisha zaidi ya watu 100 kutoka nchi 25 ni muhimu kwa wadau wote wa mbegu asili kujadiliana namna ya kuzilinda mbegu za asili.

Chilewa alisema Afrika ina changamoto kubwa ya mbegu za asili, hali ambayo itachangia kukosekana kwa uhakika wa chakula kwa siku nyingi.

"Mbegu asili zina lishe nyingi na salama kwa afya ya mtumiaji, hivyo ili kuhakikisha zinakuwa endelevu ni lazima kufanyika tafiti ambazo zitaonesha ni namna gani tunaweza kuzilinda,"alisema.

Ofisa huyo alisema iwapo serikali itafanya utafiti ambao utashirikisha wakulima ambao wanatumia mbegu asili ni wazi kuwa changamoto hiyo itapata jibu sahihi.

Chilewa alisema iwapo hakutakuwa na juhudi za kukabiliana na changamoto ya mbegu asili, ni wazi kuwa wakulima wataingia kwenye mtego wa kununua mbegu ambazo zitahitaji viuatilifu na mbolea ambavyo vina sumu na kusababisha maradhi mbalimbali.

Mratibu wa Mratibu wa Mtandao Baionoai Tanzania (TABIO), Abdallah Mkindi alisema utafiti unaonesha asilimia 80 ya wakulima wa Afrika wanatumia mbegu asili, hivyo ni muhimu kuhamasisha matumizi ya mbegu hizo.

Alisema pia utafiti umeonesha mbegu asili zina virutubisho, hivyo iwapo jamii itahamasishwa kutumia mbegu hizo changamoto ya utapiamlo ambayo inaikabili mataifa hayo itapata muafaka.

"Mbegu asili zina nafasi kubwa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yameonesha madhara makubwa duniani, hivyo rai yangu ni kuziomba serikali za Afrika kutenga fedha zitakazotumika kufanya utafiti wa mbegu hizi,"alisema.

Mkindi alisema TABIO kwa kushirikiana Mtandao wa Uhuru wa Chakula Dunia (AFSA) na SwissAid wamewakutanisha wadau hao, ili waweze kujadiliana na kutoka na kauli moja kuhusu hatma ya mbegu asili ambazo zinaonekana kupewa kisogo na watunga sera na sheria.

Kwa upande wake Mbunge wa Lindi mjini, Hamisa Abdallah alisema kilimo cha mbegu asili ndio kinaweza kuleta tija kwenye sekta hiyo, kwani historia inaonesha wazee wa zamani walitumia njia hiyo.

Hamida alisema mbegu asili hazina gharama kwenye kilimo kama ilivyo kilimo cha kisasa, hivyo ni wakati muafaka wa jamii kurejea katika mfumo huo wa zamani.

Alisema kutokana na madhara ambayo yanapatikana kwenye kilimo cha kisasa, dunia imeanza kubadilika na kutaka kurejea mifumo ya zamani ambayo ilijikita katika mbegu za asili.

"Mimi naishi na wakulima wa hali ya chini ambao anashirikiana nao kuendeleza matumizi ya mbegu asili, hivyo anaungana na wadau wengine ambao wanataka uwekezaji katika utafiti wa mbegu hizo ambazo ni salama kwa afya ya binadamu," alisema.

Alisema mkutano huo ni ujumbe sahihi kwa viongozi duniani kuweka mkazo wa kusisitiza kilimo kinachojikita katika mbegu asili ambazo ni salama kwa afya ya binadamu na mazingira.

Hamida alisema tafiti zinaonesha kuwa hata ongezeko la magonjwa duniani kwa sasa ni mengi sababu kubwa ni jamii kuacha kutumia mbegu asili kwenye kilimo.

Mbunge huyo alisema atumia nafasi yake ya ubunge kuzungumzia na kushawishi umuhimu wa mbegu asili kwenye kilimo.

Mwakilishi wa Wizara ya Kilimo, Beatrice Banzi alisema Tanzania imekuwa ikihamasisha watafiti kufanya utafiti katika sekta hiyo ya mbegu asili na mbegu zingine.

Alisema kilio cha dunia ni uwepo wa mbegu bora na salama kwa afya ya binadamu, hivyo utafiti pekee ndio unaweza kutoa jibu.

Ofisa Program wa AFSA, Famara Diédhiou alisema ni wakati muafaka kwa nchi za Afrika kuungana kuhakikisha mbegu asili zinapewa kipaumbele katika sekta ya kilimo.



Mkurugenzi Mkuu wa taasisi ya kuthibiti ubora wa mbegu Tanzania (TOSCI), Patrick Ngwediagi (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo na mwelekeo wa mwaka wa fedha 2023/24. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Wanafunzi wahimizwa kupenda masomo sayansi, teknolojia

**Na Mwandishi Wetu,** Dodoma

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imewahimiza wanafunzi kupenda masomo ya sayansi na teknolojia kwa kuwa yana mchango mkubwa wa kuleta maendeleo ya nchi.

Mkurugenzi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa wizara hiyo, Prof. Maulilio Kipanyula, aliyasema hayo jana kwenye hafla ya kugawa majarida 700 yanayofahamika kama OYLA Africa ambayo yametolewa na Kampuni ya Baobab Shalom Limited ya jijini Dar es Salaam.

Majarida hayo yalitolewa baada ya makubaliano ya ushirikiano yaliyosainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu, (TEA), Bahati Geuzye na Mkurugenzi wa Baobab Shalom Limited, Yev Semikov katika ofisi za TEA jijini hapa.

Akizungumza katika hafla hiyo, Prof. Kipanyula alisema sayansi na teknolojia imeleta mapinduzi makubwa kitaifa na kimataifa na hasa katika sekta za elimu, habari, biashara na huduma mbalimbali za kijamii.

Alisema serikali imeweka kipaumbele katika sekta ya elimu kwa kuwekeza kwa kiwango kikubwa ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, hivyo kuwahamasisha wanafunzi kujifunza kwa bidii na kuwa wabunifu.

Semikov alisema lengo la majarida hayo ni kuwezesha wanafunzi wanaoyatumia kuwa wabunifu na wadadisi kwa lengo la kuboresha maisha yao kwa ujumla.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye, alishukuru kampuni ya Baobab Shalom Limited kwa kutoa msaada huo wa majarida kupitia mfuko wa elimu unaosimamiwa na TEA.

Alisema TEA iko tayari wakati wote kushirikiana na wadau wa elimu na kuwahakikishia kuwa misaada ya elimu inayopita kwenye mfuko huo inasimamiwa kikamilifu na kutumika kama ilivyokusudiwa.





# Wasimamizi vituo vya afya wapewa somo

**Na Christina Mwakangale,** MBARALI

MGANGA Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Dk. Ray Salandi amesema wajumbe wa bodi na kamati za usimamizi wa vituo vya afya, kwenye halmashauri hiyo, wanawajibu wa kusimamia utendaji kazi wa huduma za afya ikiwamo zahanati, vituo na hospitali, bila woga.

**Sio watu wanakuja wanaondoka na dawa za kituo, zahanati au hospitali unakaa kimya, hali hii inatuharibia kila kitu.**

Akizungumza jana wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa wajumbe hao, Dk. Salandi alisema wakazi wa eneo hilo ni wanufaika wa kwanza wa huduma bora za afya, hivyo wajumbe hao wavae viatu vya usimamizi ipasavyo.

"Huduma kama nzuri utanufaika na wewe pia ambaye unaishi eneo hili, kama mbovu haathiriki mwananchi tu asiye kiongozi wote tunaathirika," alisema Dk. Salandi na kuongeza

"Sio watu wanakuja wanaondoka na dawa za kituo, zahanati au hospitali unakaa kimya, hali hii inatuharibia kila kitu," aliongeza.

Alisema kwamba, wajumbe hao ambao wamepewa jukumu hilo kisheria wasisite kufuatilia saa za kazi kwa watumishi wa umma katika zahanati na vituo vya afya, ili kuhakikisha huduma zinatolewa kwa muda uliopangwa na serikali.

"Kama mtumishi ana dharura au kuna idadi ndogo ya watoa huduma ni suala lingine. Lakini saa za kazi kwa watumishi wa umma kwa wiki hazipungui 40 hadi 48. Kufanya saa chache za kazi kunaathari kijamii," alibainisha Dk. Salandi.

Mhadhiri wa Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Dk. Ramadhani Kigume, akiwasilisha mada kuhusu uongozi alisema kiongozi aliyepewa dhamana na wananchi anapaswa kuwa mbunifu na kuja na mbinu za kutatua changamoto kwenye eneo lake.

"Uongozi ni namna ya kutatua changamoto zilizopo kwenye jamii yako, ukiwa kiongozi uwe rahisi kutumia vipaji, taaluma na ujuzi wa unaowaongoza kwa kuwaonyesha njia na siyo vinginevyo," alisema Dk. Kigume.

"Tuwasaidie wananchi kuboresha huduma za jamii, tutazitumia wote. Mfano wewe kazi yako kupita tu na gari yako V8 au yeyote mbele ya kituo, bila ya kusaidia hata kutoa ushauri wa kuboresha huduma. Ipo siku utapata ajali hatua chache kutoka kituo hicho, ambacho ulishindwa kusemea upotevu wa dawa, vifaa vichache, sasa utatibiwaje," alisema.

Mhadhiri wa Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) Dk. Cresencia Massawe, alisema wajumbe hao watoe mrejesho kwa wananchi kuhusu malalamiko yanayotolewa na wananchi, ikiwamo kauli zisizo na staha kwa wagonjwa, ili kuimarisha huduma.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na (DUCE) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na kufanyika wilayani hapa, huku yakishirikisha takribani washiriki 70, ambao ni wenyeviti, makatibu na wajumbe wa kamati hizo kutoka Hospitali ya Wilaya Mbarali, zahanati nne na vituo vya afya viwili.



Katibu Tarafa ya Mweri, Wilaya ya Ushetu, Mkoa wa Shinyaga, Tumshukuru Mudui (wa tatu kulia), akimsaidia mmoja wa wanufaika wa vifaa saidizi vilivyotolewa msaada na kampuni ya JTI Leaf, wilayani humo mkoani Shinyanga juzi, ikiwa ni sehemu ya programu yake ya kusaidia jamii mbalimbali. Kushoto ni Mbunge wa Ushetu, Dk. Emmanuel Cherehani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yataka 'speed' ujenzi Chuo cha Maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeagiza kamati ya ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Nzovwe kinachojengwa katika Kijiji cha Idiga Kata ya Bonde la Songwe Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kukamilisha haraka ujenzi ili kianze kutumika.

Serikali imeamua kujenga majengo ya chuo hicho katika eneo hilo la Idiga kwa lengo la kuhamishia shughuli za chuo hicho kutoka katika Kata ya Nzovwe jijini Mbeya ambacho yanatumika majengo ya Kanisa Katoliki.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Franklin Rwezimula wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa chuo hicho na kusikiliza kero mbalimbali za watumishi. Pia, aliagiza kasoro mbalimbali zilizobainika kwenye baadhi ya majengo zirekebishwe ili mradi huo uendane na thamani ya fedha zilizotengwa na serikali.

"Sijaridhishwa na kasi ya ujenzi wa chuo hiki, fanyeni kazi usiku na mchana ili mradi huu ukamilike kwa wakati, lakini pia hakikisheni mnajenga kwa kiwango kinachohitajika, kuna maeneo yale niliyoelekeza yarekebishwe, fanyeni hivyo haraka," alisema Dk. Rwezimula

Alisema chuo hicho kikikamilika kitasaidia vijana wanaozunguka maeneo ya vijiji jirani kupata ujuzi stahiki utakaowasaidia kujiajiri na kujipatia kipato lakini pia kitaongeza uchumi wa kijiji kutokana na mzunguko wa fedha utakaoletwa na watumishi pamoja na wanafunzi.

Aidha, alikipongeza chuo hicho kwa kutafsiri dhana ya uwezeshaji kwa vijana kwa vitendo kwa kuanzisha kozi zenye mvuto kwa vijana na kuhakikisha wanazalisha wanataaluma bora kwenye kozi wanazozitoa.

Kuhusu upanuzi wa eneo la chuo hicho, Dk. Rwezimula aliwaomba viongozi wa kijiji hicho kufanya mkutano na wananchi na kuwaomba kuongeza eneo la chuo zaidi, kwa kuwa eneo lililopo ni hekari 10 pekee ambazo hazitoshi.

Mkuu wa chuo hicho, Nickson Mandele aliiomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuongeza watumishi katika chuo hicho na kuharakisha fedha za uhamisho kwa mali za chuo pamoja na watumishi.

Mandele alisema watasimamia mradi huo ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati na wanahamishia shughuli katika eneo hilo ili majengo yanayotumika kwa sasa yarejeshwe kanisani.

Alisema kitendo cha viongozi mbalimbali kutembelea mradi huo kinasababisha kuongeza kasi ya ujenzi pamoja na kuwatia moyo mafundi.

Chuo cha Mandeleo ya Wananchi Nzovwe ni moja kati ya vyuo 55 Tanzania vilivyo chini ya Wizaraya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kusimamiwa na Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi Stadi NACTVET.

## NBS yakabidhi ramani matokeo ya sensa kwa madiwani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imekabidhi ramani za matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya ili ziwasaidie kupanga mipango ya maendeleo pamoja na matumizi bora ya ardhi.

Meneja wa Takwimu wa Taifa, Benedict Mugambi alikabidhi ramani hizo juzi kwenye hafla maalumu iliyofanyika jijini Mbeya ambapo madiwani wote 36 wa Jiji hilo walikabidhiwa.

Mugambi alisema ramani hizo zitawawezesha madiwani kutumia kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo ya kata zao ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya shule pamoja na kilimo pamoja na kutambua changamoto na mahitaji ya wananchi wao.

"Ramani hizi zinaonyesha mambo yote yaliyoko kwenye kata na mitaa, ikiwemo idadi ya watu na makazi kwenye kila mtaa, pamoja na ardhi kwa ujumla wake hivyo hata mbunge atakapokuja kwenye kata yako itakusaidia kujua na kueleza ni wapi kuna mapungufu," alisema Mugambi.

Aliongeza kuwa wanaandaa majarida yanayoonyesha takwimu za mazingira ikiwemo uharibifu wa mazingira, maeneo wanayolima kwa kiasi kikubwa , afya ya mimea, udongo wa asili, maeneo ya wilaya ambayo hayajishughulishi katika kilimo fulani lakini ardhi ya mahali hapo inafaa kwa kilimo hicho.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson alisema takwimu zinahusika kwenye mambo yote na kwamba kiongozi yeyote ili ajenge hoja zake kwa serikali kuhusu maendeleo kwenye eneo lake ni lazima atumie takwimu kuwasilisha hoja zake.



## Wataalamu maji kukutana Zanzibar, kubadilishana uzoefu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KONGAMANO la pili la maji linatarajia kufanyika leo Zanzibar, litawashirikisha watalaamu wa maji zaidi ya 400 kutoka ndani na nje ya nchi, litafunguliwa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Hassan Kaduara alitoa taarifa hiyo na kusema katika kongamano hilo watalamu wa sekta ya maji watakaoshiriki watapata nafasi ya kubadilishana uzoefu katika dhana nzima ya utafiti wa sekta ya maji pamoja na kufahamu njia mbalimbali ya kutatua kero ya maji Zanzibar.

Alisema kongamano hilo litatoa fursa kwa wadau wa sekta ya maji kutoka nje na ndani ya nchi ambao watapata fursa ya kuwasilisha ripoti za utafiti zao.

"Mwaka huu utafiti wa ripoti 64 zitawasilishwa katika kongamano hili, katika hatua hiyo kutakuwa na zawadi kwa vijana ambao ni watafiti bora" alisema.

Aidha, alisema lengo la kutoa zawadi kwa watafiti bora ambao ni vijana ni kuwahamasisha kufanya utafiti wenye kukidhi viwango ambao utasaidia Zanzibar katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta ya maji.

Aidha, alisema lengo la kushirikiana na wadau mbalimbali katika kongamano hilo ni kuongeza nguvu katika kutafuta mawazo na mbinu zitakazowezesha kuimarisha sekta ya maji nchini.

Pia alisema kauli mbiu ya kongamano hilo ni 'Kuongeza kasi ya mabadiliko: kutambua usimamizi endelevu wa rasilimali maji chini ya ardhi na huduma za maji kwa wote'.

Kongamano hilo linafanyika kwa kushirikiana na Taasisi ya Global Water Partnership Tanzania, Taasisi ya SADC Ground Water Management Instutute, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Taasisi ya Uongozi, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Chuo cha IHE-Delft.

# Somo la mazingira laanza kufundishwa sekondari

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa**

MUHEZA

SHULE ya Sekondari Shebomeza na Shule ya Msingi Antakae zilizopo wilayani Muheza mkoani Tanga ni miongoni mwa shule zinazotoa elimu ya mazingira kwa wanafunzi ili kuulinda Msitu wa Hifadhi wa Amani- Nilo unaozunguka vijiji saba katika Wilaya ya Muheza.

Elimu hiyo ni muhimu kwa vizazi vya sasa na vijavyo ili kuwa mabalozi wazuri katika kulinda msitu huo ambao unarasilimali nyingi za bayoanuai.

Akizungumza na waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari wa Mazingira Tanzania (JET) waliotembelea ushoroba wa Amani-Nilo wiki iliyopita, Bashir Mvungi ambaye ni mwalimu wa mazingira wa Shule ya Sekondari Shebomeza

**Miche ya mikarafuu wanauza kwa wananchi ambapo fedha inayopatikana husaidia katika maendeleo ya shule ikiwemo kuweka umeme wa jua ili wananfunzi waweze kujisomea nyakati za usiku.**

alisema shule hiyo inavuna utajiri kutokana na uwepo wa msitu huo.

Alisema wanawafundisha wanafunzi elimu ya mazingira kwa vitendo na nadharia ikiwemo kuotesha vitalu vya miti kama vile mikarafuu na kupanda katika eneo la shule.

Alisema miche ya mikarafuu wanauza kwa wananchi ambapo fedha inayopatikana husaidia katika maendeleo ya shule ikiwemo kuweka umeme wa jua ili wananfunzi waweze kujisomea nyakati za usiku.

Alisema mwaka jana waliuza miti ya mikarafuu na kupata Sh. milioni moja.

Alisema upandaji wa miti ya biashara ikiwemo mikarafuu na midalasini imesaidia wanakijiji kupanda miti hiyo kwa wingi na kuacha kuitumia miti ya msitu wa hifadhi kwa ajili ya kujipatia kipato.

"Kuna msemo usemao samaki mkunje angali mbichi hivyo elimu ya utunzaji wa mazingira ikianza shuleni tutakuwa na jamii yenye kujali na kuthamini mazigira," alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Antakae, Shabani Churi alisema shule hiyo inatekeleza mradi wa elimu bora ya mazingira unaofadhiliwa na shirika lisilo la kiserikali linalohusika na uhifadhi wa ndege na mazingira Tanzania (Nature Tanzania).

Alisema kupitia mradi huo walipatiwa mafunzo ya uhifadhi wa mazingira na kulazimika elimu hiyo kuitoa kwa wanafunzi shuleni hapo na kuaza kupanda miti mbalimbali ikiwemo mikarafuu.

Mkurugenzi Mtendaji wa JETI, John Chikomo, alisema elimu ya mazingira ni muhimu kutolewa kuanzia ngazi ya shuleni ili watoto waweze kuwa mabalozi wazuri wa utunzaji wa mazingira.



Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Hassan Kaduara, akizungumza na waandishi wa habari Unguja jana, kuhusu kongamano la pili la maji linalotarajiwa kufanyika leo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Dk. Mwinyi awatoa hofu wananchi kuhusu afya ya msingi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuimarisha huduma za afya ya msingi kwa maeneo yote ya Unguja na Pemba ili kuboresha huduma za uzazi salama.

Pia, imesema itaendelea kuboresha matibabu ya meno na kinywa, uchunguzi wa 'ultra sound" na huduma za maabara ili zipatikane kwa ufanisi kwenye vituo vyote vya afya.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (pichani), aliyasema hayo wakati akifungua Kituo cha Afya Bubwini Makoba kilichopo Wilaya ya Kaskazini B, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema serikali inaendelea kuimarisha miundombinu na upatikanaji wa dawa muhimu, vifaa tiba na rasilimali watu ikiwemo madaktari, wauguzi, wafamasia na wataalamu wengine muhimu wanaohitajika katika sekta ya afya.

Aidha, Dk. Mwinyi alieleza lengo la serikali kujenga nyumba za wafanyakazi kwa baadhi ya hospitali za wilaya, Unguja na Pemba ili kupunguza tatizo la makazi kwa watumishi wa sekta hiyo.



Alisema hatua hiyo itaboresha zaidi mfumo wa rufaa na kupunguza kasi ya wagonjwa kwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja na kupunguza msongamano wa wagonjwa.

Dk. Mwinyi alisema licha ya kuwepo kwa baadhi ya changamoto kwenye sekta ya afya ikiwamo uhaba wa wafanyakazi, madaktari bingwa na wabobezi kwenye kada mbalimbali za afya, hali aliyoielezea inaisababishia serikali kutumia fedha nyingi kwa matibabu ya wananchi nje ya Zanzibar.

Rais Dk. Mwinyi, alieleza katika kukabiliana na hali hiyo, serikali imeamua kushirikiana na sekta binafsi ambao wataendelea kuhudumia hospitali za serikali zikiwemo huduma za uchunguzi wa maradhi hasa kwa maeneo yaliyoimarika kwenye utekelezaji wake.

Alisema nia ya serikali ni kufikia malengo iliyojipangia ya kuwahakikishia wananchi wanapata huduma nzuri ndani ya wakati unaotakiwa kwenye hospitali na vituo vyote vya afya.

Katika hatua nyengine, Rais Dk. Mwinyi aliwaagiza watumishi wote watakaopelekwa kufanya kazi Kituo cha Afya Bumbwini Makoba wajitahidi kuitunza miundombinu iliyopo.

Pia, aliwataka kufanya kazi kwa kujitolea na huruma kwa wagonjwa na kuzingatia maadili ya kazi zao sambamba na kutumia lugha nzuri kwa wagonjwa watakaowahudumia.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmeid Mazrui alisema, ujenzi wa kituo hicho ni utekelezaji wa juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuimarisha vituo vya afya nchini.

Naye, Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Amour Suleiman, alisema ujenzi wa kituo hicho ulianza Mei 14, mwaka 2022 na kukamilika Juni mwaka huu.

Alisema ujenzi umegharimu Sh. milioni 450. 7, kwamba huduma za kliniki mbalimbali zinatolewa na kituo hicho ikiwemo huduma za wajawazito na watoto, maabara na ultrasound.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**GODLISTEN T SHIRIMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1098/0542** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MAJI YA CHAI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/269936/2023**

---

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 859 OF 2022**
**In the matter of the Estate of the Late**
**EMMANUEL FRANK SIMBUA**
**And**
**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**VALENTINO SIMBUA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate ( or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 18 day of 09 2023

**Dated at DAR ES SALAAM this 11 day of 08, 2023**

022

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NURDINI SWALEHE SALIMU** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Brast yenye namba za usajili MC 668 CER. Chassis No. NGPCJXJ5KCU03237, Engine No. 156FMIJ55201674. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/271250/202**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 22 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**NICHOLAUS MAYA MTANGI**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY STEPHEN VITALES KALAGHE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before the 7th day of Sept 2023

**Dated at Korogwe this 11th day of August 2023**

DISTRICT COURT KOROGWE TANZANIA

RESIDENT MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE DISTRICT
KOROGWE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 24 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**SALVATORY ANTHONY MTEI**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY MARRY PHILIMONI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before the ....... th day of September 2023

**Dated at Korogwe this 14th day of August 2023**

DISTRICT COURT KOROGWE TANZANIA

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE DISTRICT
KOROGWE

---

**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 48 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late of the late STIVEN PIUS MWAHESA**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration by PHILIPO EMILIAN MWAHESA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 21 day of AUGUST, 2023.

**Dated at Dodoma this 17 day of JULY, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE I/C DODOMA DISTRICT

**PRINCIPAL/SENIOR /RESIDENT MAGISTRATE**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**VERONICA GASPER MASHAMO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **KING LION** yenye usajili namba: **T 383 BYA , CHASSIS NAMBA: LDAPAK0B8BGB12667** na ENGINE NAMBA: KL162FM111146838. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/LON/RB/144496/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**
**Shauri la Madai /Ndoa Na 68/2023**
**STERIDA EXAUD TEWELE .........MWOMBAJI/MDAI**
**NWAKA EDWARD MBILINYI......MJIBU MAOMBI/MDAIWA**
**MSIMAMIZI WA MIRATHI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 15 (1)(2) ya kanuni za Mashauri ya Madai Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: NWAKA EDWARD MBILINYI WA RAMADHANI**
Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai)
Unahitajika kuhudhuria katika mahakama hii kuja kujibu dai la mdai
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 17 mwezi 08 mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 11 mwezi 08 mwaka 2023

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

---


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Japan, Marekani kuunda mfumo kuzuia makombora

**TOKYO, Japan**

TAIFA la Japan na Marekani zinatarajiwa kwa pamoja kutengeneza mfumo wa kisasa, utakaonasa na kuzuia makombora ya masafa marefu, hatua hiyo inafanyika huku hali ya wasiwasi ikizidi kuongezeka katika rasi ya Korea.

Makubaliano ya kuanza kutengenezwa kwa mfumo huo yanatarajiwa kufanyika wakati waziri mkuu wa Japan Fumio Kishida atakapofanya ziara nchini Marekani iliopangwa kufanyika Agosti 18, mwaka huu.

Rais wa Marekani Joe Biden, anatarajiwa kukutana na Waziri Mkuu Fumio Kishida na Rais wa Korea Kusini Yoon Suk Yeol, katika mkutano wa kilele wa usalama wa pande tatu, ambao utafanyika katika kambi ya David karibu na mji wa Washington Ijumaa.

Mkutano huo wa washirika hao watatu unatarajiwa kujikita kuiangazia Korea Kaskazini na mpango wake wa mara kwa mara wa majaribio ya makombora ya masafa marefu unaozidi kushamiri na kuongezeka kwa ushawishi wa China katika kanda hiyo.

Waziri mkuu wa Japan Kishida, alisema zaidi ya hayo, wanatarajia kuimarisha zaidi ushirikiano wa kimkakati kati ya nchi hizo kuhusu masuala kama kukabiliana na Korea Kaskazini.

"Kudumisha na kuimarisha utaratibu huru wa wazi wa kimataifa unaozingatia utawala wa sheria," alisema.

Mzozo kwenye rasi ya Korea katika siku za hivi karibuni unazidi kufukuta huku Korea Kaskazini ikizindua awamu nyingine ya majaribio ya urushaji wa makombora ya masafa marefu.

Maazimio ya Umoja wa Mataifa (UN) yanapiga marufuku nchi iliyojitenga kimataifa kufanya majaribio ya makombora ya masafa yoyote.

Mifumo hiyo ambayo pia ni silaha aina ya Hypersonic inamilikiwa pia na China na Russia ambayo pia Korea Kaskazini imetangaza kutengeneza, na kwamba ni ngumu zaidi kuizuia kulingana na mfumo wake wa kisasa na utendaji kazi madhubuti na kasi katika kupangua mashambulizi.

Pia inabainishwa kuwa kutokana na muundo wao, makombora kama hayo yanaweza pia kuwa na kichwa cha nyuklia.

Korea Kaskazini pia inadai kufanya majaribio ya makombora hayo ya kasi aina ya hypersonic, na kuruhusu kile kinachoitwa ndege nyepesi ambayo imeundwa kuruka kwa muda mrefu bila kutumia injini, kutoka kwenye makombora ya masafa marefu.

Chini ya mikakati mipya iliyotolewa mwezi Desemba 2022, serikali ya Kishida inaahidi kujenga jeshi kubwa lenye uwezo wa kushambulia na kuongeza zaidi bajeti katika sekta ya ulinzi.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa Japan, Marekani na Korea Kusini zimekubali kuanza kupeana taarifa muhimu, ikiwemo kuhusu urushwaji wa makombora ya Korea Kaskazini ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Baada ya tangazo la mkutano huo lililotolewa na Ikulu ya Marekani White house, Balozi wa Marekani nchini Japan Rahm Emanuel kupitia mtandao wa twitter alisema kwamba, mkutano wa washirika hao watatu utakuwa ni wa kihistoria wenye matokeo ya mabadiliko ya kimkakati kidhana.

**DW**



Kiongozi wa zamani wa chama tawala cha (UDPS), Jean Kabund, (katikati) aliyenyoosha mkono juu, ambaye waendesha mashtaka nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wameomba mahakama kumpa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu kutokana na kesi inayomkabili ya kumkashifu rais na uchochezi. **PICHA RFI.**

# Rais Tshisekedi atoa wito wa amani DRC

**KINSHASA, DRC**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Felix Tshisekedi, amesisitiza umarishaji wa amani nchini humo, huku akitoa wito kwa makundi ya waasi kuweka silaha chini na kuchagua amani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana Rais Tshisekedi, alisisitiza makundi yaliyopo kwenye majimbo ya Ituri na Kivu Kaskazini kufuata wito huo, matamshi anayoyatoa jijini Kinshasa, kukianza majadiliano kuhusu kuondolewa au kutoondolewa kwa hali ya dharura kwenye majimbo hayo.

Wajumbe 100 kutoka majimbo mawili yalio katika hali ya dharura, magavana wa zamani na wale wa sasa wa kijeshi wanashiriki katika mazungumzo hayo yanayotarajiwa kukamilika wiki ijayo.

Mwakilishi wa shirika la kiraia huko Ituri, Dieudonné Lossa, alisema kuwa wengi wanamatarajio makubwa na matumaini kuwa serikali itaondoa hali ya dharura.

"Raia wa Ituri wanataka tu jambo moja kutoka kwa serikali, kuondoa hali ya dharura." alisema Lossa.

Aidha, inaelezwa kuwa wanaharakati nao wamefanya maandamano ya kupinga kuwepo kwa hali ya dharura katika majimbo hayo ambayo pia wametaka kuachiwa huru kwa wenzao wanaozuiliwa kwa kukosoa hali ya dharura.

Ilibainishwa kuwa kutokana na ukosefu wa usalama unaosababishwa na makundi ya watu wenye silaha ambayo yamesababisha mauaji ya mamia ya raia, Mei 2021, Rais Tshisekedi, alichukua uamuzi wa kutoa usimamizi wa majimbo hayo mawili kwa magavana wa kijeshi na polisi kujaribu kukomesha ukosefu wa usalama.

Baada ya mwaka mmoja, mashirika ya kiraia yanataka kuondolewa kwa madai ya kuwa na matokeo tofauti na matarajio.

**RFI**

# Trump akabiliwa na kesi 41

**WASHINGTON, Marekani**

ALIYEKUWA Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump na washirika wake 18, wamepatikana na mashtaka 41 ya kujibu katika jaribio lao la kutaka kubatilisha matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 katika Jimbo la Georgia.

Trump na washirika wake wanashutumiwa kwa kujaribu kuvuruga matokeo ya uchaguzi katika jimbo la Georgia ambalo alishindwa na Rais Joe Biden.

Mashtaka hayo ni pamoja na kudaiwa kumshurutisha msimamizi wa uchaguzi katika jimbo hilo, anayedaiwa kuwa mwanachama wa chama cha Republican, kwa lengo la kutafuta kura za kutosha kumpa ushindi ili aendelee kusalia madarakani.

Anashutumiwa pia kuendelea kusema madai ya uongo kwamba uchaguzi mkuu ulikumbwa na udanganyifu na kujaribu kushawishi wabunge wa jimbo la Georgia kutotilia maanani maamuzi ya wapiga kura na kuchagua waidhinishaji feki wa uchaguzi kuidhinisha kwamba Trump alishinda uchaguzi huo kinyume cha sheria.

Mashtaka hayo yanaelezea namna Trump alivyojaribu kuvuruga mashine za kupiga kura katika jimbo la Georgia.

Wengine walioshitakiwa pamoja na Trump ni Mark Meadows, wakili wa Trump Rudy Giuliani, aliyekuwa mwanasheria katika wizara ya sheria wakati wa utawala wa Trump, Jeffrey Clark ambaye alikuwa mstari wa mbele katika kutaka kubatilisha matokeo ya uchaguzi katika jimbo la Georgia.

Mawakili waliokuwa wakimshauri Trump wakiwemo John Eastman, Sidney Powell na Keneth Chesebro pia wamepatikana na makosa ya kujibu.

Aidha, ilielezwa kuwa wote walioshitakiwa wataruhusiwa kujiwasilisha mahakamani adhuhuri Agosti 25, mwaka huu.

Inabainishwa kuwa waendesha mashtaka wanapanga kuanza kesi hiyo katika muda wa miezi sita kuanzia jana.

**VOA**

**Mashtaka hayo yanaelezea namna Trump alivyojaribu kuvuruga mashine za kupiga kura katika jimbo la Georgia.**

## HABARI MICHEZO




Kiungo wa Yanga, Khalid Aucho (kulia), akiwania mpira na mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis, katika mechi ya Ngao ya Jamii, Jumapili iliyopita katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga. Katika mchezo huo, ambao Simba ilishinda kwa penalti 3-1 baada ya kutoka sare tasa ndani ya dakika 90, huku Aucho akimchezea rafu mbaya Kibu ambayo inalalamikiwa kuwa ilistahili kuwa penalti halali. **MPIGAPICHA WETU**

## Yanga hasira zote CAF kwa ASAS Jumapili

INATOKA UK. 24

wanachama na mashabiki kutulia na kufurahia kikosi hicho ambacho anaamini kinakwenda kufanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na mashindano mengine ya kimataifa.

**"Tumeshaikosa Ngao ya Jamii, lakini tuna songa mbele sasa tu nageukia Ligi ya Ma bingwa Afrika, kikosi kinaingia kambini ke sho (leo), kujiandaa na mazoezi ya kimbinu na kiufundi kwa ajil i ya mechi ya Jumapili dhidi ya ASAS," alisema.**

Yanga itacheza mechi hiyo nchini, kabla ya Jumatano ijayo kuanza kampeni yake ya kutetea ubingwa wa Tanzania Bara dhidi ya KMC, mchezo utakaopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

# SABABU JONESIA KUPEWA MECHI SIMBA VS YANGA

INATOKA UK. 24

"Sisi kama kamati tunawapanga waamuzi na kule wanakokwenda kuna wadau ambao wanasimamia mashindano. Sisi hatujapata malalamiko rasmi kutoka klabu zote ila tunayasikia.

"Kama yatafika mezani kwangu na kuthibitika kuwa ni kweli, tutachukua hatua au kuendelea kuwaelimisha, lakini mpaka sasa hakuna malalamiko yoyote (rasmi). Tunayasikia na tunayasubiri yaletwe rasmi. Tunawasubiri pia wahusika wa mashindano watatuletea taarifa rasmi yapi yaliyojitokeza na yapi ya kuboresha," alifafanua Hamduni.

**MTIHANI WA FIFA**

Kuhusu madai kwamba Refa Jonesia alifeli mtihani wa utimamu wa mwili, Mwenyekiti huyo alikiri yana ukweli, lakini Shirikisho la Mpira wa Miguu barani Afrika (CAF), lilimtaka kurudia mtihani huo ndani ya wiki sita, wao wakamtaka kurudia ndani ya wiki moja, akafaulu. Jina lake litawasilishwa ngazi za juu ili kupatiwa beji ya FIFA kwa kuwa amekidhi vigezo vinavyotakiwa.

"Jonesia ni mmoja wa waamuzi zaidi ya kumi tulionao ambao wapo katika michuano ya kimataifa na orodha ya waamuzi wa FIFA.

"Awamu ya kwanza tulifanya kozi kwa ajili ya waamuzi wa kimataifa na wengine kwa ajili ya kuwaombea nafasi ili mwakani waendelee kuwa waamuzi ya kimataifa na kweli (Jonesia) hakumaliza mbio zake vizuri kutokana na matatizo mbalimbali, lakini utaratibu wa CAF ni kwamba mwamuzi yeyote wa kimataifa ambaye hakufanya vizuri anapewa nafasi ya kurudia ndani ya wiki sita.

"Sisi kama Kamati ya Waamuzi tuliwaomba waamuzi walioshindwa kufanya vizuri warudie baada ya wiki moja, walirudia na walifanya vizuri. Hata shuleni na vyuoni mwanafunzi anaweza kukosa somo moja, akarudia na akifaulu huwezi kusema alifeli mwanzo. Hivyo, mwamuzi huyo alirudia na kufaulu vizuri zaidi.

"Mwamuzi Jonesia hatuna shaka na uwezo wake. Wadau wa soka wanamfahamu kuwa mmoja wa marefa wazuri na taifa halina shaka na uwezo alionao isipokuwa ni changamoto tu zinazojitokeza kama mwanadamu," alisema.

**SABABU KUPEWA 'DABI'**

Hamduni alisema Refa Jonesia aliteuliwa kusimamia mechi hiyo ya fainali ya Ngao ya Jamii kwa kuwa ndiye Mwamuzi Bora wa Msimu Uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kanuni inawaelekeza kuwa atakayekuwa bora msimu uliopita ndiye anayepewa kuchezesha mechi ya fainali ya Ngao ya Jamii.

"Na kwa nini tulimpanga? Kwenye Ngao ya Jamii ndiyo mwanzo sahihi wa ligi kuanza na kanuni zinatueleza kwamba mwamuzi aliye bora msimu uliopita ndiye anatakiwa atufungulie ligi ili kuonesha mfano.

"Ninampongeza sana ameonyesha mfano mzuri kwenye mechi ya fainali japo kuna upungufu ambao wadau wa soka wametaja, lakini tunasubiri wasimamizi watupatie ripoti. Kama kuna upungufu, basi tutakaa naye na kuzungumza, baada ya wiki sita atakwenda kuchezesha soka nje ya nchi," alisema.

Alisema kuwa katika msimu huu wa Ligi Kuu ambo mechi zake zilianza jana, kamati imeandaa vema waamuzi kwa kuwapa mafunzo na kuhakikisha wameiva kwenye nyanja zote ikiwamo utimamu wa mwili, "kama yakitokea makosa, basi wakati mwingine yanakuwa ya mwamuzi mwenyewe".

Katika mechi hiyo iliyopigwa kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, dakika 90 ziliisha kwa suluhu, lakini Simba ilitwaa Ngao ya Jamii kwa mikwaju ya penalti 3-1 dhidi ya wapinzani wao wa jadi Yanga waliokuwa wamehodhi ngao hiyo kwa misimu miwili.

Aliwahakikisha wadau wa soka kuwa wamefanya kila kitu kuhakikisha msimu wa 2023/24 ligi inachezeshwa kwa uangalifu wa hali ya juu, viwango na ubora huku akiahidi kutofumbia macho waamuzi wote watakaovurunda.

"TFF kupitia kamati yake ya waamuzi ambayo mwenyekiti wake ni mimi, tumejiandaa vizuri na ligi, na kujiandaa kwetu ni kuwa na mafunzo. Tulianza na mafunzo ya kwanza Julai 31 kwa waamuzi zaidi ya 35 wanaohusika zaidi na beji ya FIFA. Tukapata tena waamuzi 190 kwa ajili ya Ligi Kuu na Ligi ya Championship (Ligi Daraja la Kwanza) na sasa tunaendelea na waamuzi zaidi ya 350 kwa ajili ya ligi zingine za chini," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**WEST HAM NA MAGUIRE**
KLABU ya West Ham inafikiria kujiondoa katika dili la mlinzi wa kati wa Manchester United, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 30, kwa sababu ya muda ambao inachukua kukamilisha. **(Telegraph)**

**TAH, KASSOUNOU WAWINDWA**
IWAPO uhamisho wa Harry Maguire hautatelekezwa bosi wa 'Wagonga Nyundo' hao, David Moyes, ataelekeza nia yake kwa mlinzi wa Ujerumani, Jonathan Tah mwenye umri wa miaka 27, na mlinzi wa kati wa Ivory Coast, Odilon Kossounou (22), ambao wote wako Bayern Leverkusen. **(Guardian)**

**PAQUETA KUBADILISHWA**
KLABU ya West Ham inataka kumbadilisha Mbrazil Lucas Paqueta mwenye umri wa miaka 25, na mchezaji wa Kimataifa wa Ghana na Ajax, Mohammed Kudus mwenye miaka 23, ikiwa makubaliano yafikiwa na Manchester City kuhusu ada ya uhamisho. **(Talksport)**

**BELEBA ATAKIWA BRIGHTON**
KLABU ya Brighton iko kwenye majadiliano juu ya mkataba wa pauni milioni 15 kumnunua kiungo wa kati wa Lille, Carlos Baleba mwenye umri wa miaka 19, wakiwa tayari wamekubaliana maslahi binafsi huku wakitafuta kuziba pengo la Moises Caicedo aliyeelekea Chelsea. **(Fabrizio Romano)**

**CARLOS AWANIWA LIVER**
LIVERPOOL, Newcastle United, AC Milan na Juventus ni miongoni mwa klabu ambazo zimekuwa zikimfuatilia Carlos Baleba. **(Mail)**

**GABRIEL ATAKIWA SAUDIA**
MLINZI wa Arsenal Gabriel ndiye mchezaji wa hivi karibuni zaidi anayelengwa kuhamia Saudi Arabia, ingawa 'Washikabunduki' hao hawana shinikizo la kumuuza Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 25. **(Mirror)**

**ORBAN KUMRITHI KANE**
KLABU ya Tottenham Hotspur imemtambua fowadi wa Gent na Nigeria, Gift Orban mwenye umri wa miaka 21, kama mchezaji atakayechukua nafasi ya Harry Kane baada ya kuhamia Bayern Munich**. (Football Insider)**

**FOREST YAMTAKA SYRIANOS**
KLABU ya Nottingham Forest imeanzisha tena mpango wa kufanya kazi na George Syrianos, mkuu wa zamani wa uajiri wa klabu hiyo. **(Subscription Required)**

**VILLA YAMWANIA ZANIOLO**
KLABU ya Aston Villa inakaribia kukamilisha usajili wa mkopo wa kiungo wa kati wa Italia, Nicolo Zaniolo mwenye umri wa miaka 24, kutoka Galatasaray wakiwa na chaguo la kumnunua. **(Sport Italia)**

**TIERNEY ATAKIWA NEWCASTLE**
NEWCASTLE United imewasiliana upya na Arsenal kuhusu beki wa pembeni wa Scotland, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 26, ingawa bei ya pauni milioni 30 inaweza kuwa kikwazo. **(Newcastle Chronicle)**

**CUCURELLA PIA ATAKIWA**
MLINZI wa Chelsea, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 25 pia anamvutia Kocha wa Newcastle United, Eddie Howe. **(Telegraph)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR RASMI AJIUNGA AL HILAL YA SAUDI ARABIA

Euro milioni 90 zahusika, sasa aungana na Koulibaly, Ruben Neves na Milinkovic-Savic...

**RIYADH, Saudi Arabia**

KLABU ya Saudi Arabia, Al Hilal imekubali kutoa ada ya euro milioni 90 kwa Paris Saint-Germain ili kumsajili Neymar, kwa mujibu wa ESPN.

ESPN iliripoti Jumapili kwamba mfungaji huyo bora wa muda wote wa Brazil alikuwa karibu kuafikiana na Al Hilal wakati klabu hizo mbili zilipofanya mazungumzo ya makubaliano.

Na sasa atajiunga na Al Hilal kwa mkataba wa miaka miwili na chaguo la kuongeza mwaka mmoja.

Neymar ataungana na wachezaji wenzake wapya Kalidou Koulibaly, Ruben Neves na Sergej Milinkovic-Savic, ambao wote walihamia Al Hilal mapema msimu huu wa majira ya joto.

Al Hilal ni moja ya klabu nne pamoja na Al Nassr, Al Ahli na Al Ittihad ambazo zilichukuliwa chini ya umiliki wa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia Juni kama sehemu ya kile kinachoitwa "Mradi wa Uwekezaji na Ubinafsishaji wa Klabu za Michezo."

Klabu za Ligi Kuu Saudia zimefuata mkakati mkali wa kusajili wachezaji katika dirisha hili la uhamisho, na kuwapa mkataba mnono baadhi ya nyota wakubwa wa mchezo huo.

PSG ilimfanya Neymar kuwa mwanasoka ghali zaidi kuwahi kutokea mwaka 2017 - rekodi ambayo bado anashikilia -- walipomsajili kwa kiasi kikubwa kutoka Barcelona kwa euro milioni 222.

Kuondoka kwa Neymar kutoka PSG kunahitimisha miaka sita ya msukosuko katika Mji Mkuu wa Ufaransa, Paris, ambapo mara nyingi alikuwa akisumbuliwa na majeraha na masuala ya nje ya uwanja.

Neymar ameshinda mataji matano ya Ligue 1 na mengine 13 kwa jumla akiwa na PSG, na pia kumaliza kama mshindi wa pili katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2020.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,144,1

MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
SEVILLA FC
1 | 1.38
X | 4.38
2 | 6.93

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CHELSEA YAKAMILISHA USAJILI WA CAICEDO



**LONDON, England**

CHELSEA imekamilisha usajili wa rekodi kwa England, Moises Caicedo, kutoka Brighton kwa kitita cha pauni milioni 115.

Kiungo huyo wa kati wa Ecuador mwenye umri wa miaka 21, alikaribia kujiunga na Liverpool wiki iliyopita, lakini 'The Blues' waliwazidi maarifa na kukamilisha lengo lao la muda mrefu.

Licha ya kutakiwa na 'Wekundu' hao, Caicedo alisemekana kuwa na nia ya kutaka kuhamia Stamford Bridge na hatimaye amekamilisha uhamisho huo.

Aliiambia tovuti rasmi ya Chelsea: "Nina furaha sana kujiunga na Chelsea."

"Nina furaha sana kuwa hapa katika klabu hii kubwa na sikulazimika kufikiria mara mbili wakati Chelsea iliponipigia simu. Nilijua tu nilitaka kusaini."

"Ni ndoto iliyotimia kuwa hapa na siwezi kusubiri kuanza na timu."

Akiwa mchezaji muhimu wa Brighton msimu uliopita walipofuzu kwenye Ligi ya Europa, Caicedo alikuwa mmoja wa wachezaji waliotafutwa sana kwenye Ligi Kuu England.

Kando na Liverpool, Arsenal walidhaniwa kumtamani sana mshambuliaji huyo, lakini sasa ataonekana kuimarisha safu ya kiungo ya Mauricio Pochettino huko London Magharibi.

Ni mara ya pili ndani ya kipindi cha chini ya mwaka mmoja 'The Blues' kuvunja rekodi ya uhamisho wa England, huku mshirika mpya wa kiungo Enzo Fernandez akijiunga kwa dau la awali la pauni milioni 105 Januari.

Wakurugenzi wenza wa michezo Laurence Stewart na Paul Winstanley walisema: "Moises amejidhihirisha kuwa mchezaji bora kwenye soka la Ulaya katika kipindi cha miezi 18 iliyopita na tunafuraha kumuongeza ndani ya kikosi cha Mauricio."

"Moises ana ujuzi adimu wa safu ya kiungo na ni mchezaji ambaye tumekuwa tukimlenga kwa muda."

"Tunaamini atakuwa na matokeo makubwa Stamford Bridge msimu huu - na katika miaka ijayo."

# Ten Hag ataka kusajili zaidi



**MANCHESTER, England**

ERIK Ten Hag amekiri kwamba anataka Manchester United kusajili wachezaji wachache kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili la majira haya ya joto.

'Mashetani Wekundu' hao wamekuwa miongoni mwa timu zenye shughuli nyingi zaidi katika Ligi Kuu England hadi sasa msimu huu wa majira ya joto, wakitumia fedha nyingi kuwasajili Andre Onana, Mason Mount na Rasmus Hojlund kabla ya mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu msimu huu dhidi ya Wolverhampton Wanderers juzi.

Pia kumekuwa na wachezaji wengi wanaoondoka, huku Anthony Elanga, David de Gea na Fred wakiwa miongoni mwa wachezaji walioachwa, na Harry Maguire anaweza kufuata mkondo huo.

Akizungumza katika mkutano wake na wanahabari, Ten Hag alikiri kwamba ana nia ya kusajili wachezaji zaidi.

"Siku zote nitataka wachezaji zaidi! Lakini nadhani kila kocha ungemuuliza pia angetaka zaidi. Lakini ni kuhusu mawazo; katika soka la juu tunazungumzia mahitaji, kiwango cha juu kabisa. Kwa sababu tunadai hilo kutoka kwetu," alisema.

"Tunatafuta hali kamili, lakini hupati hali kamilifu. Kisha unapaswa kuja katika nafasi yako na kufanya kazi kwa ajili hiyo, labda na si hali kamili, lakini matokeo kamili."

Maguire akikaribia kuondoka, Ten Hag anaweza kupata matakwa yake kwani karibuni iliripotiwa kuwa Man Utd wanajipanga kuingia kwenye soko la usajili kutafuta beki wa kati.

Jean Clair-Todibo, Perr Schuurs, Jarrad Branthwaite na Edmond Tapsoba wote wamehusishwa, wakati klabu hiyo pia iko kwenye mazungumzo na Bayern Munich kuhusu Benjamin Pavard.

HABARI MICHEZO

72,464/-

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/08/23 | 17:00 | Fulham FC vs Brentford FC | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 02. 19/08/23 | 19:15 | Caykur Rizespor vs Alanyaspor | 2.36 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 19/08/23 | 19:30 | Tottenham Hotspur vs Manchester United | 3.00 | 3.40 | 2.21 |
| 04. 19/08/23 | 19:30 | Empoli FC vs Hellas Verona | 2.35 | 3.15 | 2.95 |
| 05. 19/08/23 | 21:45 | Hatayspor Antakya vs Kasimpasa Istanbul | 2.32 | 3.35 | 2.60 |
| 06. 19/08/23 | 21:45 | Genoa CFC vs ACF Fiorentina | 2.95 | 3.25 | 2.30 |
| 07. 19/08/23 | 22:30 | Portimonense SC vs Boavista Porto | 2.43 | 3.10 | 2.90 |
| 08. 19/08/23 | 22:30 | CA Osasuna vs Athletic Bilbao | 2.75 | 3.05 | 2.60 |
| 09. 20/08/23 | 14:30 | VfL 1899 Osnabruck vs FC Nuremberg | 2.48 | 3.40 | 2.60 |
| 10. 20/08/23 | 14:30 | Holstein Kiel vs FC Magdeburg | 2.35 | 3.55 | 2.70 |
| 11. 20/08/23 | 16:00 | Le Havre AC vs Stade Brest 29 | 2.55 | 3.20 | 2.65 |
| 12. 20/08/23 | 16:00 | FC Lorient vs OGC Nice | 3.05 | 3.40 | 2.18 |
| 13. 20/08/23 | 17:30 | Estoril Praia vs Rio Ave FC | 2.40 | 3.15 | 2.90 |
| 14. 20/08/23 | 18:00 | Hamarkameratene vs Rosenborg BK | 2.70 | 3.25 | 2.26 |
| 15. 20/08/23 | 19:00 | FC Sudtirol Bolzano vs Spezia Calcio | 3.15 | 2.95 | 2.15 |
| 16. 20/08/23 | 20:15 | KV Kortrijk vs KAS Eupen | 2.15 | 3.45 | 3.10 |
| 17. 20/08/23 | 21:45 | RC Lens vs Stade Rennes | 2.33 | 3.50 | 2.75 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 16/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 1826 | PHU Dong FC vs Dong Tam Long AN | 2.51 | 2.92 | 2.72 |
| 13:00 | 3176 | Australia W vs England W | 3.35 | 3.20 | 2.04 |
| 15:00 | 2361 | Lee Man vs Bali Utd Pusam | 1.94 | 3.42 | 3.42 |
| 18:00 | 3453 | SFK Vrchovina vs SK Lisen | 8.54 | 5.28 | 1.26 |
| 18:00 | 4988 | FC Strani vs FC Slovan Rosice | 5.91 | 4.08 | 1.46 |
| 18:00 | 5034 | FK Jesenske vs OFK Slovenska Lupca | 2.59 | 3.35 | 2.41 |
| 18:00 | 5289 | FCI Levadia Tallinn U21 vs Viimsi JK | 3.29 | 4.28 | 1.88 |
| 18:30 | 2006 | Velke Hamry vs FK Prepere | 2.51 | 3.66 | 2.34 |
| 18:30 | 2269 | Soroksar vs Csakvari TK | 2.09 | 3.28 | 3.07 |
| 18:30 | 3099 | Shams Azar Qazvin vs Havadar | 3.65 | 2.80 | 2.06 |
| 18:30 | 4153 | AL Wakrah vs Muaither SC | 1.49 | 4.23 | 4.93 |
| 18:30 | 4406 | Teraktor Sazi vs Persepolis FC | 4.18 | 2.86 | 1.96 |
| 18:55 | 3719 | Hajer Club vs Ohud Medina | 2.04 | 2.98 | 3.53 |
| 19:00 | 1213 | TJ Tatran Bohunice vs Kromeriz | 6.53 | 5.71 | 1.30 |
| 19:00 | 1519 | Rmsk Cidlina vs FC Kolin | 5.06 | 5.06 | 1.42 |
| 19:00 | 2230 | Flora Tallinn vs Farul Constanta | 3.20 | 3.35 | 2.13 |
| 19:00 | 2906 | SK Benesov vs FK Stechovice | 2.40 | 3.52 | 2.51 |
| 19:00 | 5683 | Azam vs Kitayosce FC | 1.26 | 4.58 | 9.95 |
| 19:00 | 5832 | FK Spartak Sobeslav vs Pisek | 4.39 | 3.68 | 1.67 |
| 19:30 | 5113 | Pecs MFC vs Vasas SC | 2.70 | 3.25 | 2.27 |
| 19:30 | 5840 | Dalkurd FF vs AIK Football | 7.10 | 5.88 | 1.27 |
| 20:00 | 4170 | Budapest Honved vs Duna Aszfalt Tvse | 1.64 | 3.72 | 4.32 |
| 20:00 | 4747 | Real Madrid Castilla vs Unionistas CF | 1.91 | 3.46 | 3.46 |
| 20:00 | 5056 | Santa Clara vs SCU Torreense | 1.76 | 3.47 | 4.18 |
| 20:30 | 2104 | Sekhukhune United vs Moroka Swallows FC | 2.43 | 2.57 | 3.45 |
| 20:30 | 5931 | Al Arabi Doha SC vs Al-Shamal | 1.27 | 5.03 | 8.24 |
| 20:40 | 2949 | AL Arabi (SA) vs Jeddah Club | 2.10 | 2.97 | 3.37 |
| 21:00 | 2200 | Haukar vs Vikingur Olafsvik | 2.22 | 3.59 | 2.63 |
| 21:00 | 2603 | Thor Akureyri vs Throttur Reykjavik | 1.83 | 3.78 | 3.33 |
| 21:00 | 2883 | IF Vestri vs Afturelding | 2.98 | 3.58 | 2.02 |
| 21:00 | 3338 | UMF Selfoss vs Njarovik | 2.07 | 3.67 | 2.82 |
| 21:00 | 4445 | Magni vs Vidir | 2.44 | 3.51 | 2.46 |
| 21:00 | 3849 | Throttur Vogum vs KV Vesturbaer | 1.23 | 6.47 | 6.88 |
| 21:00 | 4716 | UMF Grindavik vs Leiknir | 2.20 | 3.64 | 2.63 |
| 21:00 | 5141 | IA Akranes vs Aegir | 1.19 | 6.46 | 8.68 |
| 21:30 | 4789 | Nueva Chicago vs San Martin SJ | 2.12 | 2.80 | 3.68 |
| 21:45 | 1001 | Boreham Wood vs Solihull Moors | 1.90 | 3.51 | 3.66 |
| 21:45 | 3875 | Kilmarnock FC B vs Dumbarton | 2.52 | 3.77 | 2.28 |
| 21:45 | 4443 | Clyde vs Stirling University FC | 2.02 | 3.61 | 3.05 |
| 21:45 | 5266 | QPR vs Norwich City | 3.28 | 3.52 | 2.02 |
| 22:00 | 2947 | Manchester City vs Sevilla FC | 1.38 | 4.38 | 6.93 |
| 22:00 | 4131 | Imbabura Sporting Club vs 9 De Octubre FC | 1.92 | 3.11 | 3.87 |
| 22:15 | 3070 | Grotta vs Fjolnir | 3.37 | 3.47 | 1.90 |
| 22:30 | 1563 | Vikingur Reykjavik vs KR Reykjavik | 1.68 | 3.71 | 4.27 |
| 23:00 | 1659 | America vs CD Alianza Cotopaxi | 2.69 | 3.46 | 2.28 |
| 23:00 | 2029 | San Martin Tucuman vs Defensores Unidos | 1.80 | 3.04 | 4.61 |
| 23:00 | 3551 | Municipal Turrialba vs AD Cariari Pococi | 3.10 | 3.61 | 2.00 |
| 23:00 | 4009 | Arbaer vs Ellidi | 1.65 | 4.59 | 3.62 |
| 23:15 | 5802 | Asociacion Deportiva Tarma vs Universitario | 3.04 | 3.09 | 2.19 |
| 23:30 | 2926 | Deportivo Moron vs CA Guemes | 1.81 | 3.28 | 4.11 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# ROBERTINHO AONYA WACHEZAJI LIGI KUU

**Na Saada Akida**




KUELEKEA mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu Bara msimu huu dhidi ya Mtibwa Sugar, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliviera, amewataka wachezaji wake kusahau furaha za ubingwa wa Ngao ya Jamii na nguvu zao kuzielekeza katika mechi hiyo.

Simba imeshafika mkoani Morogoro tayari kwa ajili ya mchezo huo wa Ligi Kuu utakaopigwa kesho katika Uwanja wa Manungu, Turiani.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema hawana muda wa kupoteza na wanatakiwa kusahau matokeo ya mechi iliyopita na kuhakikisha wanaanza vizuri ligi kwa kushinda mechi dhidi ya Mtibwa Sugar.

Alisema wanahitaji pointi tatu, hivyo wanalazimika kupambana kila mechi kuhakikisha wanapata matokeo mazuri iwe wanacheza ugenini au nyumbani.

"Wachezaji wanatakiwa kuelewa kuwa ubingwa wa Ngao ya Jamii ni mwanzo wa safari yetu ya kutafuta malengo ya kurejesha furaha za mashabiki wa Simba kwa kufanya vizuri katika michezo yote iliyopo mbele yetu.

Fainali imetusaidia kuona ubora na madhaifu ya timu yetu na tumefanyia kazi kuimarisha katika kila nafasi ikiwamo kati na safu ya ushambuliaji kuwa makini kutumia nafasi wanazotengeneza," alisema Robertinho.

Alisema anatambua msimu huu utakuwa mgumu kulingana na timu zilivyojiandaa kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri katika michezo yote ya ligi ili kufikia malengo yao.

Robertinho alisema anafahamu umuhimu wa mchezo wao dhidi ya Mtibwa Sugar ambao utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu kila timu inahitaji kupata matokeo chanya.

# Azam FC, Tabora United kivumbi Ligi Kuu Bara leo

**Na Saada Akida**

BAADA ya pazia la Ligi Kuu Bara kufunguliwa rasmi jana kwa Ihefu FC kuikaribisha Geita Gold huku Namungo ikiwa mwenyeji wa JKT Tanzania fc na Dodoma Jiji ikiialika Coastal Union ya Tanga, mtifuano wa ligi hiyo unatarajiwa kuendelea katika viwanja viwili leo.

Katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, Azam FC itaikaribisha Tabora United (zamani Kitayosce FC) ambayo ni msimu wao wa kwanza kucheza Ligi Kuu.

Mchezo mwingine utakuwa kati ya Mashujaa FC ambao watakuwa nyumbani katika Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma kuikaribisha Kagera Sugar.

Katika michezo hiyo, inapewa nafasi ya kuwa ya ushindani, kutokana na kuhusisha timu mbili zilizopanda daraja, ambapo zitataka kuonesha kwa nini zilistahili kupanda na si zingine, lakini pia usajili wao mpya ukitarajiwa kuonesha ubora wao.

Mchezo wa Azam FC dhidi ya Tabora United utapigwa saa 1:00 usiku, ukitarajiwa kuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu timu zote zinahitaji kuanza vizuri kwa kutafuta ushindi.

Kikosi cha Azam FC kinachonolewa na Kocha kutoka Senegal, Youssouph Dabo na Tabora United ikinolewa na Goran Kopunovic kutoka Serbia, ambaye amewahi kuwa kocha wa Simba Mwaka 2015 na baadaye akaondoka kabla ya kurejea msimu huu kwa jukumu la kuiongoza miamba hiyo ya Tabora.

Kuelekea mechi hiyo, Kocha Msaidizi wa Makipa wa Azam FC, Mwalo Hashim, asema baada ya kutoka Tanga ambako iliibuka mshindi wa tatu kwenye michuano ya Ngao ya Jamii, tayari wamesahau matokeo hayo na kujipanga kwa mechi yao ya ligi dhidi ya Tabora United.

Alisema mechi za Ngao ya Jamii zimewasaidia kuona madhaifu yao na kujiandaa na mechi hiyo kuweza kutumia vema uwanja wao wa nyumbani kupata matokeo chanya.

"Wachezaji wako tayari kwa ajili ya mechi yetu ya kesho (leo), tumeweleza wasahau yaliyopita na sasa kufikiria mechi ya ligi iliyopo mbele yetu dhidi ya Tabora United," alisema Mwalo.

Nahodha wa Azam FC, Sospeter Bajana alisema kilichopo mbele yao ni kusaka pointi tatu dhidi ya Tabora na kwamba mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu wapinzani wao wanahitaji alama muhimu.

Kocha wa Tabora United, Kopunovic, yeye alisema maandalizi yamekamilika na wamejipanga vizuri kuweza kupata matokeo katika mchezo wao wa leo dhidi ya Azam FC.

Alisema haitakuwa mechi rafiki kwa sababu wapinzani wao wako vizuri lakini kwa upande wao, wamejiandaa kutafuta matokeo mazuri ili kupata pointi muhimu.

"Tumejiandaa vizuri, tunatambua ubora wa Azam FC, ni miongoni mwa timu kubwa kwa hapa Tanzania, kama Tabora United malengo yetu ni kufanya vizuri na tunahitaji kuanza vizuri mechi yetu ya kesho (leo).

"Timu yetu bado ni mpya katika ligi pamoja na benchi lake la ufundi, lakini mipango yetu ni mikubwa, kikubwa ni kuhakikisha tunashinda mechi zilizopo mbele yetu ikiwamo dhidi ya Azam FC," alisema Kopunovic.

Naye Lambele Jerome, aliyezungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake, alisema wanaiheshimu Azam FC na wanaenda kufanya kile walichoelekezwa na benchi la ufundi katika uwanja wa mazoezi ili kupata matokeo

"Tunaenda kupambana kuhakikisha tunapata matokeo mazuri. Tutacheza kwa nidhamu kubwa ili kupata matokeo mazuri katika mchezo wetu wa kesho (leo), tunaenda kupambana kupata matokeo chanya," alisema Jarome.

# Michezo

Jumatano Agosti 16, 2023

Nipashe




Neymar rasmi ajiunga Al Hilal ya Saudi Arabia

UKURASA 21

# SABABU JONESIA KUPEWA MECHI SIMBA VS YANGA

## ●●●Bosi wa marefa atoa ufafanuzi kufeli mtihani wa FIFA, waamuzi waliokuwa Tanga sasa kuitwa na kamati...

**Na Adam Fungamwango**

MECHI ya fainali ya Ngao ya Jamii ya watani wa jadi, Simba na Yanga jijini Tanga, imeibua malalamiko. Waamuzi wananyooshewa kidole, wakidaiwa kutomudu mchezo.

Hoja zinazotawala malalamiko ni pamoja na mtokea benchi Kibu Denis kudaiwa kunyimwa penalti dakika chache kabla ya filimbi ya mwisho ya Refa Jonesia Rukyaa. Kiungo mkabaji Mganga Khalid Aucho anatajwa kumkwatua Kibu ndani ya boksi la Yanga.

Beki wa Kati wa Yanga, Ibrahim Abdallah Hamad, maarufu Bacca, pia anadaiwa kumpiga konzi kisogoni mshambuliaji Jean Baleke. Hivyo, kumekuwa na madai kwamba kulikuwa na ukiukwaji wa Sheria Na. 12 ya Soka (Faulo na Tabia Mbaya), lakini Refa Rukyaa na wasaidizi wake hawakuchukua hatua stahiki.

Hoja iliyoteka zaidi malalamiko hayo, ni madai kwamba Kipa wa Simba, Ally Salim Katoro, alikiuka Sheria Na. 14 ya Soka (Pigo la Penalti) wakati wa 'matuta', dakika 90 zilipotimu huku timu hizo zikiwa hazijafungana.

Sheria inasema "...wakati wa pigo la penalti, walau mguu mmoja wa kipa uwe umegusa mstari wa goli au uko juu ya mstari huo", lakini kumekuwa na madai kwamba Kipa Salim wa Simba alikiuka hilo pasi na waamuzi wa mechi kuchukua hatua.

Vilevile, kuna madai kwamba Kamati ya Waamuzi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), ilimteua Refa Jonesia kusimamia mechi hiyo ilhali amefeli mtihani wa utimamu wa mwili wa Shirikisho la Soka la Kimataifa, FIFA.

**BOSI WA MAREFA**

Katika mazungumzo maalum na Nipashe kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi, Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi ya TFF, Nassor Hamduni, alisema hawajapata malalamiko rasmi ofisini kutoka kwa klabu zote mbili kuhusu mechi hiyo. Hata hivyo, klabu kulalamikia au kupongeza uchezeshaji wa mwamuzi ni kosa kikanuni.

Hamduni, refa mstaafu aliyekuwa miongoni mwa waamuzi bora nchini mwishoni mwa 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000, pia aliiambia Nipashe kwamba hadi juzi jioni, walikuwa hawajapata ripoti ya mechi hiyo kutoka kwa wasimamizi wa mashindano.

Alisema kuwa licha ya kutopata malalamiko rasmi, wao kama wadau wa soka wamesikia malalamiko dhidi ya marefa waliochezesha mechi nne za Ngao ya Jamii na watayafanyia kazi, haijalishi watapata ripoti rasmi kutoka kwa wasimamizi wa mashindano au la. Watawaita waamuzi na kuwakumbusha majukumu yao wanayopaswa kuyafanya wakiwa uwanjani.

"Ni kweli kwenye mechi za Ngao ya Jamii kulikuwa na malalamiko kutoka kwa wadau kwamba kuna makosa yalijitokeza, lakini Kamati ya Waamuzi kazi yake kubwa ni kuwaita, kuwaelimisha na kuhakikisha wanapata elimu tosha na kuwa fiti wakiwa uwanjani.

INAENDELEA UK. 20



Jonesia Rukyaa

## Yanga hasira zote CAF kwa ASAS J'pili

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupokonywa Ngao ya Jamii na watani wao wa jadi, Simba, Klabu ya Yanga imesema kikosi chake kinaingia kambini leo huku nguvu zake zote kwa sasa zikielekezwa kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika raundi ya awali dhidi ya AS Ali Sabieh (ASAS), kutoka Djibouti itakayochezwa Jumapili katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Aidha, klabu hiyo imesema inajivunia kikosi chake baada ya kuonesha soka safi ilipocheza mechi ya fainali ya Ngao ya Jamii Jumapili iliyopita katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga dhidi ya Simba, licha ya kupoteza kwa mikwaju ya penalti 3-1.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema uongozi wa Yanga unawapongeza wachezaji na benchi la ufundi kwa kuitengeneza timu kiasi kwamba pamoja na kupoteza mechi hiyo, lakini habari kubwa ikawa ni ubora wa kikosi chao.

"Kwanza niwapongeze wanachama na mashabiki wa Yanga ambao walisafiri kutoka mikoa mbalimbali na wale wa Tanga, kuhakikisha wanaisapoti klabu yao katika mechi zote mbili za nusu fainali na fainali pia, pili tunawapongeza wachezaji wetu na benchi la ufundi kwa jitihada zao kuhakikisha timu inacheza vizuri mechi zote mbili, ni kweli tumepoteza kwa mikwaju ya penalti, lakini kiwango cha timu yetu ndicho kimekuwa mjadala mkubwa baada ya mchezo huo, tafsiri yake ni kwamba tuko tayari kwa michezo ya Ligi Kuu na ya kimataifa msimu huu unaoanza," alisema.

Ofisa Habari huyo alisema wachezaji wapya waliosajiliwa na klabu hiyo wameonesha kiwango bora, hivyo kuwataka

INAENDELEA UK. 20

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >